# *Uigaji Wa Ukristo*

Asante, Ndugu Neville. Inafahamika kuwa kundi la waimbaji watatu wa Neville ni miongoni mwa waimbaji watatu bora zaidi humu nchini. Hakika, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. [Ndugu Neville anasema, "Ninashuku hilo."—Mh.]

2 Basi ni wangapi walioyasikia yale matangazo jana? Mimi ni maskini mhubiri mkongwe, wa muda wa zaidi ya miaka ishirini, nami nimesikia mahubiri mengi. Lakini ninaamini nilisikia mojawapo ya mahubiri yanayofaa zaidi kwa siku hizi tunazoishi, niliyasikia jana, na mchungaji wetu, Ndugu Neville. Ninyi mlioyakosa hayo, mlikosa hazina kuu. Hilo liliupendeza moyo wangu. Na mke wangu alipokuwa akiosha vyombo . . .

3 Junie, nilikuwa nikimsaidia, kwa hiyo hilo halitadhuru. Delores hukufanya uvioshe, pia. Kwa hiyo . . .

4 Nilipokuwa nikimsaidia kuosha vyombo, ilibidi sote tusimame, ili tu ku—kusemezana, jinsi ambavyo Bwana alikuwa akimtumia ndugu yetu katika ujumbe wa jana kwenye redio. Nao ulikuwa ni kipeo cha ajabu, kama niliwahi kusikia kimoja. Nami nilifurahi sana kujua, ya kwamba yule ambaye Bwana alikuwa akimtumia kuuleta huo ujumbe, nilihusishwa naye, katika kazi ya Bwana. Na, kwa hiyo, na lile kundi la waimbaji wanne, ama watatu, jana, lilikuwa la ajabu kweli; nao wako hivyo, wakati wote, na vivyo hivyo na mchungaji wetu. Nasi tunathamini hili kwa mioyo yetu yote. Na kuomba ya kwamba Mungu ataendelea kuwa pamoja na ndugu yetu, na kutujalia jumbe hizi kuu zenye nguvu katika nyimbo na katika Neno, kadiri wakati unavyosonga mbele.

5 Na sasa kuninii . . . kwa sababu ya maombi yenu, ambayo—ambayo mumetuombea tulipokuwa hudumani, Bwana amebariki kwa wingi, sana. Nasi tuna furaha sana kuripoti hilo, kwamba mambo mengi Mwokozi wetu alifanya katika zile ibada; akawaokoa watu, na—nayo imani ya hao watu ikatimiza masharti ya nguvu za Mungu za uponyaji, nao wakaponywa.

6 Na sasa kwa kuwa tumepanda juu hatua moja zaidi, sasa tunaondoka tena, tukijitumbukiza hudumani juma hili lijalo, hadi Lima, Ohio, kwa Wabaptisti, ambapo bila shaka tunahitaji maombi yenu kwa—kwa ajili ya mkutano wa Lima juma hili.

7 Halafu tutoke huko, turudi twende Evansville, Indiana, kwa usiku mmoja tu, hiyo ni tarehe tatu ya—ya Februari, kwa Wafanyabiashara Wakristo . . . wanaanzisha tawi jipya, nami ninapaswa kuzungumza asubuhi. Kisha jioni, ikiwa theluji haianguki au hali mbaya ya hewa, ili niweze kurudi, vema, nitabaki kwa ajili ya ibada jioni hiyo. La sivyo, nitakuwa hapa maskanini usiku huo, Bwana akipenda, tarehe tatu Februari.

8 Kisha, tarehe kumi hadi kumi na saba, ni huko Minneapolis. Na tarehe kumi na sita, asubuhi ya tarehe kumi na sita, ni kiamshakinywa cha Wafanyabiashara Wakristo. Na kwa hiyo tu—tunatarajia wakati mzuri sana kwenye—kwenye kiamshakinywa hiki, kwenye kiamshakinywa hiki, na pia mkutanoni.

9 Tutarudi, kwenda Shreveport; kisha kwenda Phoenix, Arizona, kwenye Bustani ya Madison Square. Na huko kwa ushirikiano kamili, pamoja na wahudumu wote wa Shirika la Bonde la Maricopa, kwenye ile Bustani kubwa, nzuri ya Madison Square, kule Phoenix, tuna ibada.

10 Halafu basi, kutoka huko, hadi kwenye Bonde la San Fernando, pamoja na Ndugu Espinoza, pamoja na watu wote wa Meksiko. Na halafu hadi kwenye ziwa fulani, (nasahau), Ziwa Clear, kwa siku tatu usiku kule juu. Na kisha kuingia Oakland, basi, kwenye Ukumbi mkubwa mzuri wa Civic ambao huketi karibu watu elfu kumi, pamoja na Shirika la Wahudumu wa Twin City linaloufadhili huo mkutano. Ambao, tunamshukuru Mungu, na kuomba ya kwamba atatupa umwagikaji mkuu wa baraka Zake.

11 Muhtasari tu kutoka kwa katibu wangu, kidogo tu. Mnaona, sina budi kukisukumia mbali kutoka kwangu. Mimi . . . Vema. Naam, ni mtu fulani kuniona baada ya mkutano. Baadhi ya wahudumu wameingia, ndugu wa Martin. Vema, ndugu, tutaona mara tu baada ya ibada, kwenye chumba cha mashemasi.

12 Sasa, ninalipenda Neno, kwa sababu Neno ndilo Ukweli wa Mungu. Basi nilikuwa nikizungumza jana na nanii wangu . . . Ndugu yetu Cox, na Dada Cox. Nami nafikiri kwamba ndugu . . . Naam, yuko asubuhi ya leo, na sijui kama Dada Cox yuko, ama hayuko. Lakini tulikuwa tukijadili baadhi ya mambo ya maisha ya Kikristo, kama Wakristo wafanyavyo wanapokutana pamoja. Na, katika hayo mazungumzo, yakatokea, juu ya kunena juu ya, kuwakashifu raia wenzetu wa Ufalme. Jinsi ambavyo tunasikia matangazo wakati mwingine, ambayo yanamkata jamaa huyo mwingine vipande-vipande, na kutaja majina yao, na—na kuwaambia wao si Wakristo, na kadhalika. Ambao, ni watoto tu. Hivyo tu. Hao ni watoto tu. Nasi tunapaswa kuwa watu wazima. Hiyo ni kweli. Na, kwa hiyo, watu wazima hawazungumzi namna hiyo. Sisi . . .

13 Lakini, tulikuwa tunazungumza, na, mimi pamoja na Ndugu Cox, nami nikasema, "Vema, nimekusudia moyoni mwangu kuhubiri dhidi ya dhambi, dhambi tu. Nami ninaiweka wazi tu. Na popote pale i—i—ilipo, Mungu anaweza—anaweza kuiweka mahali pake."

14 Mvulana m—mdogo, wakati mmoja, huko chini kusini, kulikuwako na m—msemo, kwamba alikuwa amepiga magoti kwenye safu ambapo alikuwa akilima. Na wakati ka—kasisi

mmoja alipopitia hapo na kumsikia huyo jamaa mdogo akizikariri alfabeti, "A, B, C, D," kadhalika, naye alikuwa amepiga magoti, kwa hiyo huyo kasisi alifadhaika sana. Kwa hivyo akamsikia huyo mvulana mdogo akikariri alfabeti, na kisha anasema, "Amina."

15 Basi wakati akiinuka, mbona, yule kasisi akanena naye, na kusema, "Mwanangu, mimi ni m. . . mtumishi wa Bwana. Nami nilikusikia ukiomba, lakini ulikuwa tu unakariri alfabeti. Nami si—sielewi ni kwa nini ulikuwa tu ukizikariri alfabeti."

16 Akasema, "Bwana, si—siwezi kuomba." Akasema, "Si—Sijawahi kuomba. Lakini, nilikuwa na mama na baba waombaji, ambao tayari wamekwenda Mbinguni." Kisha kasema, "Mama, mimi . . . Yeye alikufa nilipokuwa mvulana mdogo sana. Lakini nakumbuka nikimsikia alipokuwa katika shida, alimwendea Bwana, na kuomba. Naye alikufa nilipokuwa mdogo sana, asingeweza kunifundisha kuomba. Nami nimetiwa mikononi mwa mtu asiye na huruma, anayenipiga na kunitesa. Nami ni—nilikuwa . . . niliwazia, labda, nikiisha kujifunza ABC zangu, kama ningeweza kuyachukua ma—maneno yote na kuzikariri herufi zote, labda angeweza kuziweka pamoja na kuelewa nilichomaanisha."

17 Hayo ndiyo maombi ya uaminifu. Bila shaka Yeye angeweza kuziweka pamoja. Sio jinsi tunavyoomba, katika midomo yetu, ni nia ya mioyo yetu, ndiyo Mungu anayosikia. Wakati mwingine haisikii midomo yetu; anasikia nia yetu, kile, nia ya moyo wetu.

18 Kwa hiyo, katika kufanya hivyo, jana, niliguswa sana wakati huu, na kwa kuwa ni humu maskanini, ninaweza kueleza baadhi ya mambo ambayo nilikuwa nikifikiria, yapate kuwa msaada au manufaa. Na kama nikipata kusema jambo lolote lisilo jema, bila shaka ni—nisingependa kulimaanisha hivyo, ikiwa lilikuwa ni kinyume na imani ya mtu fulani. Lakini ningelielezea tu kama—kama upendo, na ningependa, labda, kujaribu kulinyoosha. Kama vile watu wasioamini katika uponyaji wa Kiungu, na kadhalika. Nawe hukuamini, mbona, mimi . . . nami kusema ninauamini, inge—isingekuwa kwamba nilikuwa nikijaribu kubishana nawe, lakini nilikuwa nikijaribu kulielezea kwa—kwa wale wanaouamini; kama mnaelewa tu ninachomaanisha.

19 Sasa, nikiomba kwamba Mungu ataelewa, najua anaelewa. Anaelewa; tunajua hilo. Sasa, nilikuwa nikizungumza na mtu msomi sana kutoka Canada. Na kama tunavyojua, Wakanada ni . . . Ikiwa unawajua, umewahi kuwa na uhusiano wa kibinafsi nao, wao ni wasomi, wa kina sana, wengi wao. Wala hawana matatizo huko juu tuliyo nayo huku. Na mle ndani, niliona ya kwamba mtu huyu, hata hivyo, hana umri mkubwa sana kuliko mimi, labda ana umri wa miaka hamsini, naye alikuwa ameingia mvi kabisa, na masharubu yake yalikuwa ya mvi, na, hata hivyo,

umri haujazidi miaka hamsini. Nami nikamwambia, "Ndugu yangu," alipokuja kwenye chu—chumba nilichokuwa nikikaa. Mchungaji wa ka—kanisa, nikasema . . . nikamtazama.

20 Na miaka michache tu iliyopita, huko Saskatoon, tulipokuwa na mkutano mkubwa wa pamoja kwenye ule uwanja mkubwa wa maonyesho, nilipoingia kwenye mikutano ya uinjilisti, alikuwa na nywele nyeusi. Masharubu yake yalikuwa meusi. Naye alikuwa . . . alikuwa na binti wawili wachanga, nao wameolewa sasa na wana watoto.

Na kwa hiyo nikasema, moyoni mwangu, "Loo, imekuwaje?"

21 Akasema, "Ndugu Branham, yapata miaka miwili iliyopita, nilifikiri labda Bwana alikuwa ameniita Marekani kwa—kwa kazi." Akasema, "Nikaenda Pwani ya Magharibi, nami nikashikana na matangazo fulani yanayoenezwa kote nchini." Naye akasema, "Nilipoona jinsi walivyotumia kwa udanganyifu fedha walizotumiwa," akasema, "Kamwe nisingeweza, kama Mkristo, kukaa pale tena. Nikaondoka. Ndipo nikaungana na lingine." Kisha kasema, "Ilikuwa ni kutoka kwenye kikaango kuingia motoni." Naye akasema, "Ndipo basi niliweka na kugundua mambo mengi sana," kisha kasema, "kugundua udhaifu wa mimbara ya Marekani!"

22 Nami nikasema, "Ndugu, hiyo ni kweli. Hatuna tabaka la katikati hapa, la kuzungumzia. Sisi—sisi ama tuna walio baridi kwelikweli na wa kawaida na wasiojali, au mlokole aliyekiuka mpaka. Wala hatuna walio katikati." Nami nikasema, "Ni—ni vibaya sana."

23 Naye akasema, "Kisha nikaja hapa." Kisha akasema, "Ndugu Branham, mara nilipofika hapa, na ujumbe wangu wa kwanza, niliona ilikuwa ni kupiga kinanda, na kupindua viti. Ndipo," akasema, "ndipo nikaanza kushangaa." Kisha akasema, "Ndipo, kupitia hayo yote, nilijaribu kuhubiri Injili, katika Neno tu. Basi ilipohubiriwa," akasema, "Mimi . . . Kulikuwa na kitu kingine, kwamba baada ya muda kidogo Bwana aliniruhusu kupenya kwenye upako na kuleta . . . Roho Mtakatifu akaja miongoni mwetu na upendo. Nayo amani ya Mungu ikaanza kumiminika juu ya hilo jengo."

24 Kisha kasema, "Ndipo nikasema, 'Sasa, Roho Mtakatifu yuko hapa, nasi sasa tutamwabudu Bwana na kuyaweka maisha yetu wakfu kwa Mungu.'"

25 Kisha kasema, "Mvulana fulani mdogo, asiye na hekima ya kutosha angalau kuingia mlangoni, akakimbia mimbarani. Akasema, 'Amina, mhubiri! Hiyo ni kweli. Tazama, mafuta yamekuwa yakitiririka kutoka mikononi mwangu, asubuhi nzima. Haleluya! Acha watu waje hapa, nami nitatoa mafuta haya ya upako kwa ajili ya uponyaji.'"

26 Akasema, "Ndugu Branham, nikasema, 'Mwanangu, tafuta kiti uketi.'"

27 Ndipo kasema, "Unajua nini kilichotukia? Mzee kiongozi akaniambia, '*Wewe* jitafutie kiti uketi.'"

28 Akasema, "Tutawezaje kamwe . . . Unawezaje, au wahubiri wanaojaribu kushikilia msimamo huo kati ya hao walokole wawili, kuusawazisha mzigo?"

Nikasema, "Neema tu ya Mungu." Loo, ni mahali pa namna gani!

29 Ndipo huyo mtu akatupa mikono yake usoni mwake na kulia, mpaka, mimi na mke wangu tumesimama pale, na machozi yakitiririka kwenye miguu ya suruali yake. Akasema, "Ndugu Branham, ninaelekea Saskatoon, nitoke kwenye mchafuko huu wa pepo mchafu."

30 Nami nikasema, "Hiyo ni kweli. Vikundi vya Kimarekani vya kijamii, vya kielimu, vimepingana sana na wenzao. Nalo hilo kundi lingine limeingia katika mambo ya ajabu-ajabu mpaka, Injili ya kweli, ni vigumu kupata mahali pa kukaribia, na kuchukua mamlaka."

31 Lakini, wakati nikiondoka nyumbani, nikizungumza na Ndugu Cox, nilipokuwa nikishuka barabarani, hajui lolote kuhusu hili, anapoketi hapa, chini barabarani, nilisema, "Bwana, jinsi hayo yalivyo kweli! Na jinsi imekuwa vigumu, kujaribu kuwapelekea watu Injili ya kweli, kuvuta kutoka pande zote mbili, na kujaribu kushikilia katikati ya barabara, kama vile tumeshindania kutoka hapo tangu saa ile jiwe la pembeni lilipowekwa." Mnaona? Sasa, na baadhi . . .

32 Nikasema, "Vipi kuhusu hawa Wamarekani hapa chini? Itakuwaje kwao?" Na ilionekana kana kwamba Kitu fulani kilisema . . . kikazungumza tu nami, na kusema, "*Wewe* unafanya nini? Hili linakuhusu *nini*? Nifuate *Mimi*."

33 Ndipo lile ono likarudi niani mwangu, ile siku nilipoweka jiwe la msingi. Niliporudi nyumbani, nilikuwa nikimnukulia mke wangu. Ni wangapi wanaokumbuka lile ono la ile asubuhi ya jiwe la msingi? Limewekwa pale pale kwenye jiwe la msingi sasa, miaka ishirini na mitatu iliyopita, nafikiri. Na lilikuwa . . .

34 Nilikuwa tu ng'ambo ya barabara hapa, nikiamka tu asubuhi moja, yapata saa moja, katika Juni wakati jiwe la msingi lilipowekwa, naamini, ama Julai. Na kwenye hiyo asubuhi, nikitazama mawio ya jua la mashariki, nilikuwa nikimsifu Bwana, kwa sababu hiyo maskani ingekuwa basi . . . ingewekewa jiwe hili la msingi. Bw. Marcum na hao wengine walikuwa hapa, na wengi wao walikuwa wameuchimba huo msingi, na kadhalika. Nami nilipaswa kuweka jiwe la msingi. Tunazo picha zake, na kadhalika. Na kila mtu alipaswa kuweka katika jiwe hili la msingi, ishara fulani ndogo, na hata Wakatoliki walipita pale na kutia ndani maskini shanga zao na kadhalika, chochote walichokuwa nacho, kwenye jiwe la msingi.

35 Lakini asubuhi hiyo, Roho Mtakatifu aliniambia, nilipokuwa nimelala pale. Nilienda . . . Katika siku hizo, sikujua kuliita ono. Nilisema tu ilikuwa ni mpagao. Ndipo nikaona ono lililonena na kusema ya kwamba kazi yangu itakuwa kati ya hivyo vitengo viwili vya Kipentekoste, cha utatu na cha umoja, na kulikuwa na mahali patupu kwa kila upande kujazwa. Sikuikingama. Nilivunja tu kutoka kwa kila mti na kuupanda chini. Na hiyo miti mikubwa ikaelekea mbinguni, ikikua upesi, nayo matunda yakaanguka chini, nayo yalikuwa matamu. Nilikuwa nikiyala. Na pale msalabani, hapo mbele yangu tu, pote palifunikwa na matunda.

36 Ndipo nilipofika mahali pale, Roho Mtakatifu akashuka juu ya hiyo miti na kusema, akiitikisa na kunguruma, Naye akasema, "Fanya kazi ya mwinjilisti." Kasema, "Utakapotoka katika hili, soma Timotheo wa Pili 4." Kasema, "Fanya kazi ya mwinjilisti. Hii siyo maskani yako." Nami nikasema, "Wapi . . . " Nami nikaiona hii maskani kama ilivyo leo hii.

Nikasema, "Iko wapi maskani yangu?"

37 Naye akaniketisha chini ya mbingu angavu ya bluu. Naye akasema, "Fanya kazi ya mwinjilisti. Timiza huduma yako. Maana utakuja wakati watakapokataa Mafundisho yenye uzima; bali watajikusanyia pamoja, waalimu, kwa kuwa wana masikio ya utafiti, nao wataiondokea ile Kweli, wazigeukie hadithi za uongo."

38 Kama hilo halijatokea, neno kwa neno! Ndiyo maana nimejaribu kulishikilia Neno kwa dhati. Na hilo ndilo somo langu usiku wa leo, "Juu ya Neno!"

39 Sasa, asubuhi ya leo, kwa neema ya Mungu, ningependa kuliendea somo lingine. Lakini kabla ya kuliendea hilo, wakati mkifungua Ezekieli mlango wa 6, ningetaka kusema hivi, ya kwamba, katika kukaribia, kila mahali, nimejaribu sana kulidumisha Neno ipasavyo. Kwa hiyo, niombeeni ili daima niwe mwaminifu kwa Neno. Jambo ndilo hilo: kwa Neno! Vema.

40 Sasa, katika Ezekieli, mlango wa 36, nasi tungetaka kuanza kusoma kwenye kifungu cha 26.

> Roho mpya na *moyo mpya . . . nitawapa* ninyi, . . .

41 Halafu basi katika cha 27:

> *Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, . . .*

42 Sasa na tuinamishe vichwa vyetu kabla tu hatujakaribia jambo hili.

43 Baba yetu wa Mbinguni, leo, ni kwa mioyo ya shukrani, tunapoukaribia wakati huu mtakatifu kwa utulivu na kwa uchaji, kwamba wakati, tunajuaje kama saa ii hii huenda ikaamua kikomo cha Milele cha mtu anayeketi hapa! Na thamani ya nafsi hiyo inalinganishwa na maelfu mengi ya

ulimwengu. Kwa hiyo tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utaturuhusu tukaribie kwa kicho, kwa uchaji, na kwa mtazamo wa maombi.

44 Na pia, kunaweza kuwa na wagonjwa wameketi sasa, ambao, leo hii, katika msimamo wao wanaopokea kupitia Neno hili, unaweza kuamua ni muda gani zaidi watakaa duniani. Kwa hivyo tunatambua ukuu wa muda uu huu.

45 Nasi tunaomba ya kwamba Uwepo Wako mkuu utatupaka mafuta sisi sote, kwa kuwa sisi ni watu wa duniani, Wewe umetutoa ardhini, na ardhini tutarudi. Na ni wakati tu tunapoishi katika chombo hiki cha ardhini, tunayo majaliwa ya kukutumikia Wewe, na kuwaleta wengine Kwako. Kwa hivyo tunaomba ya kwamba uiruhusu mioyo yetu isalimishwe kwa Neno Lako, na jalia Roho Mtakatifu alichukue Neno na kulikabidhi kwetu kadiri ya uhitaji tulio nao. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao mpendwa. Amina.

46 Kama yanibidi kutaja. . .kwa dakika chache, asubuhi ya leo. Mke wangu aliniambia hivi majuzi, kasema, "Billy, kama ungeweza kupunguza mahubiri yako kufikia dakika thelathini, badala ya saa mbili na dakika thelathini, nafikiri yangekuwa na ufanisi zaidi."

47 Nami nikasema, "Kadiri ninavyokupenda, na kadiri ninavyojua kuwa hiyo ni kweli, lakini, unaona, sina mwingine wa kuniongoza ila Roho Mtakatifu."

48 Wala sijui zaidi ya kuendelea kuzungumza tu anapoendelea kulisukuma mbele, kwa hiyo hivyo ndivyo ninavyopaswa kufanya. Na hata ninaposimama, wakati Yeye anabariki, na wakati habariki, basi mimi ni mtu mwenye mashaka, na kusanyiko langu vivyo hivyo; na kila mhudumu mwingine anayezungumza kwa uvuvio.

49 Lakini kama somo langu lingekuwa, asubuhi ya leo, kama ningeliita hivi: *Uigaji wa Ukristo*. Uigaji wa Ukristo!

50 Katika Maandiko hapa, ambayo ni Neno la Mungu, tunasoma hapa ya kwamba nabii, ambaye alikuwa amenena juu ya siku mpya. Sasa, Ezekieli alikuwa akitoa unabii, ama akitabiri yale ambayo yangetukia katika wakati ujao, si katika wakati wake.

51 Lakini, nabii ni mwonaji, naye anaitwa, katika Biblia, tai anayeenda juu sana angani. Na kadiri unavyopanda juu zaidi, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi.

52 Kwa hiyo, tai hupaa juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote. Hakuna ndege anayeweza kuenda pamoja na tai. Wala hakuna jicho kama la tai. Mwewe hana nafasi machoni pake. Wala mwewe asingeweza kustahimili mwi—mwinuko wa mahali ambapo tai anaweza kupaa. Angekufa. Yeye hana. . .Hana maumbile aliyo nayo tai.

53 Sasa, mwewe ni ndege, kadhalika na nde—ndege wengine, lakini tai aliumbwa hivyo kwa sababu yeye ni ndege anayeruka juu sana. Naye anaweza kwenda juu sana mpaka anaweza kuona vitu ambavyo ndege wengine hawawezi kuona, kwa sababu yuko juu zaidi. Basi, Mungu, katika kumwumba tai, alimwumba kwa kusudi hilo, kwa maana kiota chake kiko juu zaidi kuliko vingine. Maskini makinda wake wako kwenye kiota, na wanakula ardhini. Kwa hivyo, ili kuona dhoruba, au matatizo yakija, tai, ili kujihami, hana budi kwenda juu zaidi, apate kuwalinda makinda wake.

54 Naye Mungu alimfananisha nabii na tai ambaye angetokea katika umbo la nabii. Yeye ni mwo—mwonaji, ambaye, katika Roho, hupanda juu kupita mhemko wa kanisa. Anapita mdundo wa muziki. Anapita kupiga makofi. Anapita furaha kati ya watakatifu. Anapita hayo yote. Mungu humleta katika milki fulani peke yake, peke yake. Kisha Yeye anamfumbua jicho, Naye anamruhusu atazame huku na huku na kuona mambo yajayo. Kisha anamrudisha chini, kati ya washiriki wa huo mwili, ili kuwatabiria juu ya kile kilicho karibu kutukia.

55 Kwa hiyo, Mungu alikuwa amemchukua Ezekieli, juu, juu sana, na kumwacha aone kote, yapata miaka elfu mbili mia sita. Wazia hilo. Sasa, na kumwacha awe na . . .

Na—nabii pia ni karama ya maarifa. Maarifa ni . . .

56 Kama vile wakili, anayevisoma vitabu. Nawe unapoenda kumchukua wakili wa kuitetea kesi yako, yeye anachukua tu anachojua, nawe unamlipa kwa kile ajuacho, kuwasilisha kesi yako mbele ya hakimu.

57 Na, sasa, karama ya maarifa, katika Biblia, ni unabii, ambayo hupanda juu na kuyaona mambo haya yajayo, na kuyarudisha chini tena. Lakini hayana budi kulingana na Biblia, pamoja na Kitabu. Kama yako nje ya Kitabu, basi hayapokelewi, kwa maana Hakimu anatoa hukumu kwa Kitabu. Mnaliona? Kwa hiyo lazima yawe kwenye Neno.

58 Halafu, Neno ambalo Mungu amenena kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, si kwamba Mungu anazungumza na kumwambia nabii jambo fulani wakati huo, ni kwamba nabii anashika kile ambacho Mungu amekwisha kusema, kwa maana hilo Neno lilikuwako kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu alinena Neno, nalo liko huko nje kabisa, limetandazwa, kwa wakati. Ndipo nabii anapanda juu na kuuona wakati ujao. Kwa hiyo, ni karama tu ya maarifa, ambayo yeye huishusha chini, na kuiweka kwenye karatasi.

59 Sasa, Ezekieli, nabii, anapanda juu na kuiona siku tunayoishi. Loo, ni safari ya jinsi gani kuipanda ngazi ya Yakobo! Kuona kimbele yale yatakayotukia, naye anayashusha chini, na katika miaka hii iliyopita, miaka elfu mbili iliyopita . . .

ambapo Ezekieli aliishi yapata miaka mia sita au mia nane kabla ya Kuja kwa Kristo.

60 Walikuwa na moyo mgumu. Na, huo ulikuwa, Roho Mtakatifu asingeweza kuuingia moyo huo. Hakuwa na njia ya kuuingia moyo huo, kwa sababu ulikuwa wenye dhambi. Na kulikuwako tu na upatanisho wa damu ya mnyama, uliokuwa kati ya moyo huo mgumu na Muumba. Lakini wakati damu hiyo ya mnyama, ikiwa ni kibadala, bila shaka, bali ni kivuli tu, ama mfano, wa ile Damu ya kweli ijayo. . .Ambayo, ule uhai katika chembe ya hiyo damu ulikuwa ni uhai wa mnyama, ambao haungeweza kupatana na roho ya mwanadamu kwa sababu uhai wa mnyama hauna nafsi ndani yake, lakini uhai wa mwanadamu una nafsi ndani yake, kwa hiyo, basi, visingeweza kuchanganyikana, kama vile mafuta na maji. Lakini Kristo alipokuja na akafa, na sasa Damu ya Kristo, ambayo ilimwagwa pale Kalvari, ndani ya chembe hiyo ya Damu mnakaa si mwingine ila Uhai wa Mungu. Mnaliona?

61 Angalieni. Basi mwabudu huja mbele za Mwenyezi Mungu na Damu hii ifaayo, iliyotengwa, ni Damu ya Mkombozi inayotukomboa. Ulijiweka kwenye duka la rehani, kwa dhambi; Adamu alikuweka kwenye duka la rehani. Lakini Kristo alikuja, na Yeye ndiye Mkombozi wako, nawe ni wa Kristo. Mungu alikukabidhi kwa Kristo, kama zawadi ya upendo kwa ajili ya dhabihu Yake. Nawe unaletwa kwa Kristo na Roho Mtakatifu aliyekubembeleza kupitia Damu ya Bwana Yesu, na kukuwasilisha Kwake kama zawadi. Naye Mungu anapenda karama Zake, Naye hatavumilia kuziona zikiharibika.

62 Mhudumu mmoja alimwuliza mwenzake, hivi majuzi. Ambalo, sasa samahani hili, hili lina sehemu ndogo tu ya Fundisho langu mwenyewe ndani yake, lakini huku maskanini sisi hufanya jambo hilo.

63 Sasa, jamaa mmoja alimwuliza mwenzake, hivi majuzi. Akasema, "Unaamini. . .Huamini kama mtu aliwahi kuwa mtoto wa Mungu, aliyezaliwa na Roho wa Mungu, akaoshwa kwa Damu na kukombolewa kabisa na Mungu, kwa kufanywa upya moyo wake, kwa kuoshwa kwa maji, kwa Damu, kwa njia ya Neno, na kufanyika mtoto wa Mungu; hudhanii mtu huyo angeweza kutenda dhambi na kumwacha Mungu, ambapo angepotea?"

64 Naye huyo mhudumu, aliyekuwa akizungumza, akiwa ni mwanafunzi mzuri sana wa Biblia, alisema, "Nitalijibu swali lako ukilijibu langu. Unafikiri kwamba mtu angeweza kuwa mzuri sana, hata asiseme uwongo, asiibe, wala kufanya jambo lolote baya, lakini angekuwa mwema sana hata Mungu angempokea Mbinguni bila Damu ya Kristo?" Hapana, bila shaka sivyo.

65 Usingeweza kwenda Mbinguni bila Damu ya Bwana Yesu, haijalishi wewe ni mwema kiasi gani. Ni haki tu ya kujibunia. Wala hatuendi Mbinguni kwa haki ya kujibunia, haijalishi wewe ni mwema jinsi gani. Haiwezekani kabisa kwako kwenda Mbinguni kwa wema wako.

66 Ni rehema ya Mungu iliyokununua pale Kalvari, nawe ni zawadi ya upendo wa Mungu kwa Kristo. Na kama Mungu alimpa Kristo za—zawadi, Kristo huitunza zawadi Yake. "Wote wanijiao Mimi, wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna hata mmoja wao anayepotea. Nitawafufua katika siku za mwisho."

67 Sasa, unaweza kuchochewa kihisia. Unaweza kuwa na mafuta yakipitia mikononi mwako, ama kunena kwa lugha, au kucheza katika Roho, ama kujiunga na kanisa, ama baadhi ya mambo ya ajabu-ajabu ya siku hizi, na unaweza kupotea, bila shaka. Hiyo ni kweli. Lakini kama wewe ni zawadi ya upendo wa Mungu kwa Kristo, uko salama.

68 Sasa, maisha yako yatathibitisha kile ulicho. "Kwa matunda yao mtawatambua." Kama unajaribu kujifanya kuwa mpole na mnyenyekevu, na kadhalika, basi bado ungali nje ya Ufalme. Sio. . . Ni matendo yako mwenyewe basi.

69 Na hapo ndipo kanisa, hao watu, wanaojiita kanisa, wameshindwa vibaya sana, kwa sababu ni katika matendo yao wenyewe ambapo wanajisikia kwamba wanastahili fadhili na neema ya Mungu, kwa yale wafanyayo na jinsi wanavyoishi. Lakini hayo hayana uhusiano wowote nalo. Ni zawadi ya Mungu. Dhamiri yako mwenyewe kukuepusha na kuzimu ingejaribu kukufanya, ama ungekwepa kuzimu, hasa, ingejaribu kukufanya uishi vyema na kuwa sawa. Raia mwema atafanya hivyo, na si lazima awe Mkristo. Nimewaona watu wengi, ambao hata walilikana Jina la Bwana Yesu, walikuwa watu wazuri; hiyo inamaanaisha, kibinadamu.

70 Angalia jinsi Esau alivyokuwa mtu bora zaidi kuliko Yakobo. Lakini hakuwa na dhana ya kujua kwamba alikuwa ameuza haki zake za mzaliwa wa kwanza. Maana, alizidharau, naye akakataliwa machoni pa Mungu; ambaye alikuwa muungwana zaidi sana, na jirani, na m—mtenda kazi, kuliko vile Yakobo alivyokuwa. Yakobo, jina lake lenyewe ni mtwaa mahali pa mwingine. Mnajua *mtwaa mahali pa mwingine* ni nini? Ni "mdanganyifu." Basi hiyo—hiyo. . . Na, lakini, Esau alikuwa muungwana, katika kila hali.

71 Lakini, Yakobo alikuwa na shauku kubwa ya haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza. Na bila kujali mtu yeyote alimwita nini, kama ningelisema, kunradhi usemi huo, wangeweza kumwita, "mtakatifu anayejibingirisha, mlokole," ama chochote walichotaka kumwita, lakini yeye aliiheshimu haki hiyo ya

mzaliwa wa kwanza. Hiyo ndiyo nia yake yote. Haidhuru ilimgharimu nini, alitaka hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza.

72 Sasa angalieni, sasa, katika kulikuza kanisa. Sasa, kama kanisa linajumuisha tu. . . Kama Mwili wa Kristo utaongozwa tu na wasomi, theolojia, mawazo ya kiakili, basi tunategemea kabisa maarifa ya kiakili ya mwanadamu. Kama nikiliweka wazi hilo. . . Kama kanisa linawategemea tu wenye akili, ama jinsi mtu huyo angeweza kuliweka kanisa, na kujenga mahali pakubwa, na kurembesha viti, na kinanda cha bomba cha maelfu ya dola, na jinsi ambavyo angeweza kuhubiri ujumbe wake kwa njia ambayo inge—ingewaleta watu kanisani, na kujiunga na kanisa; na kadiri wafuasi walivyo wengi kwenye kitabu, ndi—ndivyo, ndivyo walivyo wengi Mbinguni.

73 Sasa, na—nawatakeni mpate hili, wala kamwe msiliache liponyoke. Ikiwa tunahitaji tu mawazo ya kiakili ya mwanadamu, hatumhitaji Roho Mtakatifu. Ikiwa kanisa litaendeshwa na kutawaliwa kiakili, mpango wa kielimu, na juu ya akili za wanadamu, hatumhitaji Roho Mtakatifu. Na iwapo litaendeshwa na Roho Mtakatifu, hatuhitaji mambo ya kiakili. Ni ama moja au nyingine.

74 Sasa, mihemko ya kiakili, sasa, kama tukininii tu, "Kadiri mtu angekuwa mwerevu, ndivyo alivyo na akili, kadiri alivyo na elimu, ndivyo anavyoweza kutumia sarufi bora zaidi, ndivyo kanisa lilivyo bora zaidi, ndivyo watu walivyo bora zaidi." Ikiwa anaweza kuwasilisha mpango, na kusema, "Sasa tutajenga kanisa kubwa. Tutaliita jina fulani. Tutavutia usikivu wa watu, kote jijini, tunapopiga kengele kila Jumapili asubuhi, kwenye mnara-pia wetu. Tutavutia usikivu wa maskini, mwenye dhambi aliyepotea, katika ufukara, anapoona kwamba tunavaa nguo bora zaidi; anapoona kwamba wanawake wetu wanaweza kuzirembesha nywele zao, wanawake maskini wanaweza kuona jinsi wanawake wetu wanaweza kutengeneza nywele zao, zile kofia nzuri wanazovaa. Basi tunapowasilisha hili kwa watu, maskini na wenye njaa watahudhuria mikutano ye—yetu nao watatamani kuwa kama wanawake hawa walivyo. Nao wanaume wataona jinsi tunavyovaa suti nzuri, na jinsi tunavyovalia, na jinsi. . . magari tunayoendesha, na yale tufanyayo, na jinsi tunavyosimama katika matabaka ya kijamii ya jijini, pamoja na Kiwanis na vilabu vingine, na mambo tunayojiunga nayo. Wataona kuwa wao. . . halafu ma—maskini na wasiojua kusoma na kuandika watakuja na kutamani kuwaleta watoto wao na kuwaelimisha, ili waweze kuwa wanachama wa jumuiya hii kuu inayoitwa kanisa." Sasa, kama huo ndio mpango wa Mungu, wako sahihi. Lakini Yesu hakulinukuu hivyo.

75 Yesu alisema, "Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu." Kwa hiyo, kupitia miradi ya elimu ya ulimwengu, ambayo ni sawa, ni sawa kama haitaliacha Hili nje. Lakini mwanadamu havutwi kwa Kristo kwa mambo ya kiakili, kwa

theolojia. Roho Mtakatifu, pekee, ndiye nguvu za Mungu za kuvuta. Maskini hawatalipokea kamwe, na matajiri hawawezi, mpaka wawe maskini wa mambo haya ya ulimwengu. Kristo, akiwa tajiri, alifanyika maskini, ili kwa umaskini Wake tupate kuwa matajiri. "Ajikwezaye atadhiliwa; naye ajidhiliye atakwezwa." Wamekivuruga hicho kitu chote. Wanajaribu kuwaingiza watu kanisani, kwa hotuba za kiakili. Tunachohitaji sio hotuba za kiakili. Lakini, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na nguvu na maonyesho na madhihirisho ya Roho, ndiyo tunayohitaji kuwaleta watu kanisani. Ni upako wa kuvuta wa Roho Mtakatifu.

76 Shule na seminari ni nzuri sana, sina neno dhidi yazo, lakini huo sio mpango wa Mungu. Mungu aliwachagua wajinga na wasiojua kusoma na kuandika, watu ambao wasingeweza kuzungumza vizuri, watu ambao hata wasingeweza kusoma jina lao wenyewe. Kama Biblia ilivyosema, "Walikuwa wasio na elimu wala maarifa." Lakini walikuwa wametoka kwenye shule bora zaidi. Kwa kuwa walipomponya yule mtu kwenye lango liitwalo Zuri, walitambua kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Hiyo hapo Shule.

77 Na katika jambo hili, kwa kuwa tuna makanisa ya kiakili siku hizi Marekani na ulimwenguni kote, tunapofika kwenye shule ya aina hiyo, basi Mkristo, mwaminio, mshiriki wa kanisa, akisoma Biblia yao, anaona kwamba hana budi kujaribu kujifanya mnyenyekevu, hana budi kujaribu kuwa hivi. Lakini, kwa kufanya hivyo, anafanya tu uigaji wa kimwili. Acha hilo lizame kwa kilindi. Mlinganisho wa kimwili! Anajaribu kutenda jambo ambalo kweli haliko moyoni mwake. Moyoni mwake anawaza jambo moja, na kujaribu kutenda lingine. Ambalo, katika lugha halisi ya kweli, hiyo inamfanya mnafiki.

78 Yesu alisema, "Enyi wanafiki, mwawezaje kunena mema? Maana kutoka katika hazina ya moyo kinywa hunena." Ikiwa huneni kulingana na yaliyo moyoni mwako, moyo wako unawaza jambo moja nawe unazungumza lingine, hilo linakufanya mnafiki.

79 Neno lenyewe *Farisayo* linamaanisha "mwigaji." Waliigiza dini yao, kwani walikuwa na moyo wa jiwe. Walikuja na kusema, "Bwana Mwema, tungetaka kuona ishara kutoka Kwako, kuthibitisha ya kwamba Wewe ni kile ulichosema."

80 Kasema, "Mnaniitaje mwema? wakati hakuna mtu aliye mwema ila Mungu." Akasema, "Kizazi dhaifu na cha zinaa chatafuta haya. Na kutakuwapo na ishara watakayopewa. Kama vile Yona alivyokuwa ndani ya tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi, siku tatu mchana na usiku."

81 Sasa, kujaribu kuweka mpango huu mpya, maafikiano haya mapya ambayo Mungu anayo pamoja na kanisa, ambayo

yaliwasilishwa huko Pentekoste; si ya kiakili, hata kidogo. Lakini, watu mia moja na ishirini (wavuvi, watengeneza mahema, na wake wa nyumbani) walipanda katika chumba cha juu na kungoja mpaka unabii wa Mungu ulipotimia, nao wakapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

82 Yesu alisema, “Acheni mahubiri yenu. Msiende mbele zaidi. Msifanye chochote cha zaidi juu yake. Lakini ngojeni katika mji wa Yerusalemu, mpaka, mpaka mtakapovikwa Nguvu zitokazo Juu.”

83 Sio, “Mpaka mtakapopokea B.A. yenu, au D.D. yenu, au chochote kile; mpaka mtakapokuwa na Ph. D., saikolojia.” Sio, “Na, kuwa, utakapokuwa mwalimu wa kiakili, lakini ngoja hadi upate diploma yako.” Sio, “Ngoja mpaka utakapopewa shahada.”

84 Lakini, “Mpaka mtakapovikwa Nguvu zitokazo Juu,” sio kutoka shuleni, lakini, “zitokazo Juu. Ndipo mtakuwa mashahidi Wangu, katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata sehemu za mwisho za dunia.”

85 Agizo Lake la mwisho lilikuwa, “Ulimwenguni kote; mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, naye asiyeamini atahukumiwa. Na,” kiunganishi, “ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; katika Jina Langu watatoa pepo; nao watanena kwa lugha mpya; au wakinywa kitu cha kufisha, au wakishika nyoka, havitawadhuru; na wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Katika mfano kama huo, ulikuwa uwe ndio ishara ya mwaminio, badala ya wenye elimu na wenye akili, kwa sababu mwenye akili hawezi kutoa hayo.

86 Sasa tunaona, basi, kuchukua. . . Alikuwa anaenda kutengeneza Kanisa jipya. Hakutaka. . . Huwezi kuling’arisha kanisa la kale. Unalifanyia tu ukarabati, wala halifai kitu. Ni moyo mpya. “Nitaondoa moyo wa kale wa jiwe.” Sio, “Utautupilia mbali.” Lakini, “Nitauondoa.” Je, mnaona tofauti yake? Ni tendo la neema. “Nitauondoa.”

87 Nanyi watu, Baptisti, na ninyi Presbiteri, mnaohubiri usalama wa Milele na kutenda kama ulimwengu; aibu kwenu! Mnahubiri nini? Bila shaka.

88 “Nitatoa moyo wa kale wa jiwe na kuweka moyo wa nyama ndani.” Sasa angalieni. Alisema angefanya hivyo. Kama huwezi kuliweka Hilo, kuzungumza Hilo, katika kanisa la kale la kiakili.

89 Na hiyo ndiyo sababu Marekani iko katika hali iliyomo siku hizi, kwa sababu imekaushwa kwa wazo la kale la kiakili. Hiyo ndiyo sababu haina budi kujitokeza, na—na inamlazimisha kila mtu kutia sahihi karatasi, na kadhalika, kwa ajili ya maskini uamsho wake wa Hollywood unaokuja. Nao wote wanatoka, na kama wasichana warembo na wavulana, na kuweka programu ndogo. Na wanapoondoka, wanarudi na kuona ya kwamba

karibu asilimia tisini waliomkubali Kristo kama Mwokozi, hawapo tena.

90 Kuna nini? Haukuwa uamsho. Ulikuwa ni udanganyifu wa kiakili. Hiyo ni kweli. Iliwasilisha tu jambo fulani, wakati Wamarekani wakifanya upumbavu na kupiga makofi yao, na—na Holly-. . .makala ya televisheni. Tumeigeuza kuwa te—televisheni. Mimbara imeshushwa ikawa sanduku la mtindo wa Hollywood. Wakati, yule mhubiri wa Injili wa mtindo wa kale, ambaye alikuwa akinywa maji ya birika, na kuhubiri usiku kucha kwa mwanga wa taa; imebadilishwa. Lakini, tumeibadilisha, na ndiyo maana tumepata kundi la wasomi.

91 Basi utapataje, katika mahali ambapo kila nyumba inaonyesha televisheni ikiwa na *Ni Nani Anayempenda Lucy* na vipindi hivi vingine vyote vipotovu hewani na kwenye televisheni, na vitu kama hivyo, tutaiwasilishaje Injili hii mpya jinsi Kristo alivyotwambia tufanye, katika kitu kama hicho? Kama nia ingali ni ya kimwili, itapitia katika mambo ya ajabu-ajabu na ulokole. Italikwepa Neno la Mungu na kukimbilia mdondoko wa mafuta na chochote kile. Sasa utalizuiaje? Biblia ilisema itakuwa hivyo, kwa hiyo huwezi kulizuia. Hakika. Mungu alisema itakuwa hivyo. Sasa tunaelekea wapi?

92 Wasomi! Bikizee, wanampodoa uso; angali ni bikizee yule yule. Mzee, wanamfanyia ukarabati; yeye ni mzee yule yule. "Nitafungua ukurasa wangu mpya, kwenye—kwenye Mwaka Mpya, kisha nitaanza maisha mapya. Nitatupa kiko changu," na kukiokota kesho yake. Mnaona? Huyo ni wewe tu. Sio ukarabati; ni Kuzaliwa, ndiko kanisa linakohitaji.

93 Sasa huwezi kuhubiri Hili katika kanisa la kale. Halitalivumilia. Yesu alisema hayo katika Luka, yapata mlango wa 5, kuhusu divai katika viriba. Alisema, "Huwezi kuweka divai mpya katika viriba vikuukuu. Ukifanya hivyo, vitapasuka."

94 Hilo lilikuwa likinishangaza, hilo lilikuwa likiistaajabisha akili ya—yangu ya ujana, nilipokuwa nikiwazia, "Kiriba kinawezaje kupasuka?" Sasa kile tunachoita chupa, ikiwa kuukuu, haileti tofauti yoyote, kwa sababu ni kioo.

95 Lakini, katika wakati wa Yesu, kile alichokuwa akizungumzia, kilikuwa ni chupa ambayo walitumia wakati huo, ambayo ilitengenezwa kwa ngozi ya mnyama. Nayo ngozi ya mnyama ilikuwa imetengenezwa. Ndipo wakati ngozi ya mnyama ilipozeeka, mbona. . .Wakati ilipokuwa mpya na changa, na ilikuwa tu imetengenezwa hivi punde, ilikuwa inanyumbuka. Lakini ilipozeeka, ilikauka. Sasa, wengi wenu ninyi watu mnajua ngozi ni nini inapokauka. Inazeeka na kukauka, na yote imesinyaa na ni ngumu sana. Sasa, ukiweka divai mpya ndani ya hicho, haina uhai wowote ndani yake; itapasuka.

96 Ni kama tu kujaribu kuhubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, katika nguvu halisi za—za ufufuo, ni kujaribu kuweka jambo hilo mbele ya watu. Unapofanya hivyo, inakuwaje kama ukiitia ndani? Hiyo divai mpya ina Uhai, nayo Divai mpya ingali inachachuka. Loo, natumaini mnaliona. Uhai mpya unachachuka.

97 Hiyo divai mpya ingali inachachuka. Basi kama iko katika kiriba kipya, ambamo mafuta ya huyo mnyama yangali katika hiyo ngozi, wakati divai mpya inapoanza kusukuma nje, hiyo ngozi itanyoka.

98 Vinginevyo, wakati Biblia iliposema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," hiyo ngozi mpya itasema, "amina," inyoke pamoja Nayo. Na wakati Divai mpya inaposema, ya kwamba, ubatizo wa Roho Mtakatifu, "Mimi ndimi Uzima wa Mungu unaofanya kazi ndani yako," hiyo ngozi mpya itasema, "amina," ijinyoshe Kwayo. Wakati Divai mpya inaposema, kwamba, "Roho Mtakatifu anatosha kwa ajili ya uponyaji wetu leo hii," divai mpya itajinyoosha yenyewe, Divai ikiwa ndiyo Neno. Na inaposema hivyo, basi ile chupa mpya itasema, "amina," ijinyoshe Kwake.

99 Lakini ule mwili wa kale utafanya nini? "Siku za miujiza zimepita na zimetoweka." Basi, tunafanya nini? Je, tunafanikisha nini? Sisi ni . . . Yeye alisema, "Chupa kuukuu itaangamia, na divai itaangamia pamoja nayo." Na ni karibu kama kutupa lulu zako mbele ya nguruwe. Wanageuka na kuzikanyaga chini ya miguu. Je, mnaliona?

100 Sasa, Kristo hawapaki mafuta wahudumu kuihubiri Injili ili tu irudi Kwake bure. Lakini, Yeye anakutarajia ulipokee Neno. Na unapolipokea Neno, uwe tayari. Chukua ngozi hiyo kuukuu ya ng'ombe uliyokuwa ukiishi ndani yake huko, hiyo hali baridi ya kale, na uibadilishe na ngozi ya kondoo ambayo inaweza kunyumbulika kwa Neno la Mungu. Kila kitu Biblia inachosema, utaitikia, "Amina." Lakini lazima kitoke katika Biblia.

101 Kwa maana, divai mpya huchachua tu divai. Inathibitisha tu vi—vipengee vilivyomo. Chachu husukuma tu tunguu la pombe, ambalo hufanya msururu wa kupasuka, chachu inapopasua maskini povu hii, kuifanya kamilifu zaidi; kuipa ladha bora zaidi, kuipa mshiko mzuri zaidi, kuifanya iwe na nguvu zaidi, kuifanya isiweze kuchachuka. Amina.

102 Ndipo wakati chachu ya elementi ya mwanadamu, ambayo imeletwa katika Divai mpya, inayotaka kupasua hiyo povu, kueneza nguvu zake za pombe; inasukumia mbali, kutoka kanisani, elementi zote za kilimwengu namna hiyo, na kulihifadhi kanisa.

103 Juisi ya zabibu itachachuka katika muda wa saa ishirini na nne, bali divai haitachachuka kamwe, maana chembechembe

ya uhai imo ndani ya divai, ikichachuka, na kusukuma, na kusafisha vijidudu. Na kadiri inavyozidi kuwa na umri mkubwa, ndivyo inavyozidi kuwa bora zaidi. Hayo yatosha.

104 Divai mpya, inaweza tu kuwekwa kwenye viriba vipya vya kipentekoste. Mungu alikuwa navyo mia moja na ishirini vilivyokusanyika katika chumba cha juu; baada ya kuvipaka mafuta kwa Neno Lake, navyo vilikuwa vimelainika, na kujifanya upya na kutoa uothodoksi wote wa kale kutoka kwavyo, wa mfumo wa kale. Basi Mungu alikuwa na viriba mia moja na ishirini vimewekwa kwenye chumba cha juu, wakati, huku wameinua shingo zao juu, na faneli upande wa juu.

105 Ndipo Roho Mtakatifu alipoanza kumwagika, viriba hivi vilipata uhai sana, mpaka vikaanza kutoka nje mbio, vikihubiri Injili, vikirukaruka mahali mahali. Ndipo kimoja kikaruka kwenye kisiki na kusema, "Hili ndilo lile," akarudi moja kwa moja pamoja na Neno. "Hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, 'Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamwaga Roho Yangu, Divai Yangu mpya, katika miili Yangu mipya.'" Ni uamsho wa jinsi gani waliokuwa nao! Huo ndio utaratibu wa Mungu.

106 Hivi hapa vikaja viriba vyake kadhaa, vikipasuka, na hapo alilala mtu anayeteseka. Basi wakati mtu huyu anayeteseka alipougusa mkono wa mmoja wa hawa, mbona, mateso yake yakamwacha. Naye akapata baadhi Yake, akaanza kurukaruka na kumsifu Mungu, na kukimbia hekaluni, akipaza sauti, na kumtukuza Mungu.

107 Huo ndio utaratibu wa Mungu; si shule kubwa iliyo na digrii, bali tukio hai tendaji, la Roho Mtakatifu; si ulokole, bali Roho Mtakatifu wa kweli, halisi, akitenda kazi. Hebu mlione, ndilo ombi langu.

108 Sasa angalieni mpangilio wa Maandiko. Ni mkamilifu. Mungu alisema, "Kwanza, nitaondoa moyo wa kale wa jiwe; huwezi kupokea chochote. Kisha," akasema, "Nitawapa roho mpya." Sasa, huyo si Roho Mtakatifu.

109 Hapo ndipo kosa limefanywa. Wengi wa watu, watu wengi, hasa, wanakuja madhabahuni kuomba, nao wanashuka mle kuomba, na, katika kuomba, wanaanza kujisikia vizuri kidogo. Wanaweza kusimama na kuendelea, na kurukaruka huku na huku kwa muda kidogo, na baada ya muda unakuta wanaruka tu, wanarukaruka, wanarukaruka...?...wanarudi tena. Kamwe hawakumpokea Roho Mtakatifu. Haijalishi wanarukaruka jinsi gani, au walipiga mayowe kiasi gani, au ni kiasi gani wao...mafuta yalikuwa yametokea mikononi mwao, ama walikuwa na nyuso zilizojaa damu, ama walinena kwa lugha kiasi gani, ama walipaza sauti kiasi gani, ama—ama yale waliyofanya. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Hiyo

ilikuwa tu ni mihemko ya kibinadamu. Walipata roho mpya, nao wanamfurahia.

110 Nitasema jambo fulani, nami ninataka lizame kilindini, basi Mungu na asaidie. Kuna u—upande wa kimwamsho wa lile linalojiita kanisa la Roho Mtakatifu siku hizi. Wamejenga ulokole mwingi sana, na kukimbia huko nje, kwa sababu wanalipuuza Neno. Wanaenda tu, pamoja, "Loo, tulikuwa na mkutano mzuri sana! Haleluya! Haleluya! Haleluya!" Sasa, unapofanya hivyo, wala huzai tunda la Roho, basi . . . Uko katika roho mpya. Hukuzoea kufanya hivyo, hiyo ni kweli, lakini ilibidi Mungu akupe roho mpya. Mbona, roho uliyokuwa nayo, hata usingeweza kuendana na nafsi yako, kwa hiyo utamvumiliaje Mungu?

111 Kwa hiyo, ilimbidi Mungu kukupa moyo mpya, sio uliotiwa kiraka. Moyo mpya; hizo ni akili zako unazowazia nazo, njia mpya ya kuwazia. Ndipo, anapokupa njia mpya ya kuwazia, "Naam, hiyo ni kweli. Biblia inaonekana kuwa ya maana. Nilikuwa siamini Hiyo. Ninaiamini sasa." Sasa, huo hapo uamsho wako mkuu. Unaona? Wanasema, "Naam, hakika, sitaki kwenda kuzimuni. Nataka kumkubali Kristo." Hilo ni sawa. Hilo ni zuri. Hiyo ni hatua yako ya kwanza tu.

Kisha akasema, baada ya hayo, "Tena nitakupa roho mpya."

Ni kitu gani hicho? Shauku mpya. "Nataka kufanya mema."

112 "Sasa, najua mimi ni Mkristo. Sina budi kuninii . . . Nitavuta sigara moja zaidi, na kisha nitaitupilia mbali." Mnaona? "Nami nita—nita—nitaona tu. Nita—nita—nitakaa tu nyumbani usiku wa leo, mwajua. Nitaninii tu . . . " Vitu hivi vyote vidogo "tu, tu," ndivyo hasa. Hawa alisimama kwa muda kidogo tu. Hayo ndiyo yote yaliyompasa kufanya.

Lakini, sasa, hiyo ndiyo roho mpya.

113 Basi angalieni mpangilio wa Maandiko. Baada ya kutoa moyo mpya, na roho mpya, alisema, "Kisha nitaweka Roho Yangu." Sasa nini? Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema hapa. Huo ndio mpangilio, nambari, mpangilio wa nambari wa Maandiko, "Moyo mpya; roho mpya; na halafu Roho Yangu." Kisha, Roho Mtakatifu wa Mungu . . .

114 Moyo mpya wa Mungu aliouweka ndani yako, unakaa moja kwa moja katikati yako. Hiyo ni ninii yako—msukumo wako, ambapo wewe—wewe . . . ninii yako—mihemko yako inatoka. Nayo hiyo roho mpya inakaa moja kwa moja katikati ya huo moyo mpya. Naye Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu, anakaa moja kwa moja katikati ya roho yako mpya. Na, hapo, anadhibiti mihemko yako.

115 Ni kama tu sp—springi kuu katika saa maarufu, nayo inajitia majira yenyewe. Sio lazima uizungushe kila siku. Mungu aliizungusha mara moja, kwa yote. Nayo imewekwa moja kwa

moja katikati ya . . . ya maisha ya—yako, ya maisha yako mapya. Na kama springi kuu, inapoendelea, na kupiga taratibu, hiyo saa, inadhibiti kila chembe ndogo ya saa hiyo, kwa wakati mkamilifu.

116 Na wakati Roho Mtakatifu . . . Sio digrii mpya, sio kanisa jipya, sio wazo jipya, si mhemko mpya, si mafuta mapya, si dansi mpya, si midomo mipya, si lugha mpya, si *hii* mpya, si kofia mpya! Lakini Mungu anapoweka Roho Yake katikati ya roho yako mpya, basi huna haja ya kujifanya mpole, huna haja ya kutenda kama Mkristo. Inadhibiti kila kitu kilicho ndani yako. Inakupa adabu, inalifanya kanisa kutenda kazi kwa utaratibu, inazifanya karama kufanya kazi kikamilifu. Na kama itabidi uondolewe mahali unapofikiri unapaswa kuwa, na kuwekwa mahali pengine, inakudhibiti.

117 Sio kuruka-ruka, "Kamwe sitarudi tena." Hapana, bwana. Hiyo inaonyesha kuwa ile springi kuu haimo humo. Unapolipuka kwa kila jambo dogo linalotukia, unatia sumu tabia hiyo. Ndipo ikitokea mchungaji agonge kitu kilicho katika Neno, nawe, "Puuff! Vema, siamini Hilo." Kuwa mwangalifu, ewe ngozi ya kale ya ng'ombe! Unaona? Jihadhari. Ile springi kuu mpya haijawekwa humo ndani vizuri, bado.

118 Lakini, inadhibiti. Inakufanya uamini. Inakufanya utende kwa njia fulani mpaka unakolea chumvi. Nao ulimwengu mzima unaona kiu ya kuwa kama wewe. Huyo ni Roho Mtakatifu anayekaa katikati ya roho yako. Ndiye springi kuu. Hapo ndipo ile nira, ambayo umefungwa nayo . . .

119 "Loo, nachukia sana kwenda kanisani, usiku wa leo. Sininii . . . Na, mhubiri huyo, kama hakuchosha kwa maneno mengi sana, ningetaka kumsikia kwa dakika chache. Lakini, nakwambia, mara ya mwisho nilipoenda, niliposhuka kwenye karamu ya kadi, Susie aliniambia, 'Je, unataka kuniambia, huo ujasiri wenyewe, ya kwamba umejidhili mwenyewe, kuzishusha nywele zako? Unataka kuniambia ya kwamba hutavaa hizo kaptura tena, Lydia?'" Vema, unaona, jambo ni kwamba, kama umepata tu roho mpya, itakuua tu. Hiyo ni kweli.

120 Lakini unapokuwa na Roho Wake, inafanya kila mhemko kupiga tu vema kwa Neno la Mungu. Utapiga moja kwa moja pamoja na Neno. Utasema, "Vema, sasa, Susie, hebu kidogo. Biblia ilisema, 'Ni chukizo mbele Zake, kufanya hivyo.' Nao upendo wa Kristo umeingia moyoni mwangu, nami ninampenda kupita kiasi kufanya jambo hilo. Unaona, ninampenda Yeye."

121 "Yohana, unataka kuniambia kwamba umehusishwa na kundi hilo la walokole, na hutavuta sigara kwa sababu mvulana mpya amezaliwa nyumbani kwangu?"

122 "Lakini, unaona, Yohana, inasema ya kwamba hatuna budi . . . Roho Mtakatifu, moyoni mwangu, ananiambia kwamba

tunapaswa kujiepusha na uchafu wote wa dunia.” Mnaona? Mnaona?

123 Sio, “Yohana! Haleluya, Yohana! Utukufu kwa Mungu, Yohana! Bwana asifiwe! Unaona mafuta hayo mkononi mwangu! Utukufu kwa Mungu! Yohana, naweza kunena kwa lugha. Haleluya! Nitaninii . . . ” Hapana, hapana. Hivyo sivyo Roho Mtakatifu anavyojiendesha Mwenyewe. Hapana, hapana.

Anajiendesha kwa adabu.

124 Paulo aliposimama mbele ya Agripa na kulileta Neno, alisema, “Ee Agripa . . . ”

125 Naye Agripa akasema, “Paulo, karibu unishawishi kuwa Mkristo.”

126 Akasema, “Agripa, je, ni jambo lisilosadikika kwako, ukiwa Myahudi, kwamba Biblia tayari imesema na kuzungumza juu ya Yehova? Je, ni neno lisilosadikika kwamba Mungu angewafufua wafu?”

127 Sio, “Agripa! Haleluya! Utukufu kwa Mungu, Agripa! Haleluya!” Hapana, huo ulikuwa ni wazimu.

Lakini, “Agripa, Maandiko yanasema.”

128 Unaona mahali ile springi kuu inapopiga kukuelekeza? Moja kwa moja nyuma. Huna haja ya kuwa na wasiwasi juu yake. Yote yako katika mpango wa Mungu. Inapiga kukurudisha nyuma moja kwa moja. “Usiwazie utakayosema,” alisema Yesu. “Sio wewe unayenena. Ni Baba yako anayekaa ndani yako. Ndiye anayenena.”

129 “Agripa, wewe ukiwa Myahudi, na unazijua torati zote za Agano la Kale, je, ni neno lisilosadikika kwako, Agripa, kwamba Mungu anawafufua wafu?”

Agripa akasema, “Paulo, kusoma kwingi kumekugeuza akili.”

130 Akasema, “Sina wazimu, Agripa, bali niko hapa tu kukwambia yale Mungu amefanya katika Neno.” Mnaona?

“Loo, umekuwa mtakatifu anayejibingirisha, Paulo.”

131 “La, Agripa, ninasema tu yale Mungu aliyosema hapa katika Maandiko, ya kwamba angemfufua Mwanawe, Kristo Yesu, katika siku za mwisho. Na sasa, Agripa, lingekuwa jambo lisilosadikika kwako, kwamba Yehova Mungu, aliyeifungua Bahari ya Shamu, aliyeileta miujiza katika siku hizo, kwamba asingefanya miujiza leo hii?”

132 Akasema, “Paulo, karibu unishawishi kuwa Mkristo.”

133 Paulo akasema, “Laiti ungelikuwa kama nilivyo mimi, ila tu kwa minyororo hii ambayo nimevaa hapa mikononi na mguuni mwangu.”

134 Huo ndio wakati ile springi, katikati ya roho mpya katika moyo mpya, inapofanya kila mhemko kujidhibiti wenyewe. Mnaona ninachomaanisha? Haya basi. Hapo ndipo, ambapo, unapokiondoa kichwa chako kutoka kwenye nira ya ulimwengu.

135 Kasema, "Nitaenda huko na kujiunga, lakini nakwambia. . . " Na kuingiza kichwa chako katika nira pamoja na Kristo? Ati unasema ulifungwa nira pamoja Naye? Halafu unaanza, "Loo, inaumiza mabega yangu. Inaidhuru heshima yangu ya kijamii. Watu nilioshirikiana nao wakati mmoja, hunipita na kusema, 'Naam, yule pale! Yeye ni mtakatifu anayejibingirisha.' 'Yule pale anaenda. Mnaona, yeye, Yohana haji kwenye chumba cha karata tena.' Loo, ni ninii tu. . .Loo, inanidhalilisha, Ndugu Branham." La. Hukupata kitu sahihi.

136 Wakati springi hiyo kuu iko katikati, ikipiga vizuri, basi nira imelainishwa manyoya. Loo, jamani! Haijalishi ulimwengu unakuita nini, haileti. . .

137 "Loo, nilirudi nyuma, kwa sababu, nakwambia, nisingeweza kuvumilia wakiniita *hiki, kile,* na *kinginecho*." Vema, kamwe hukuwahi kupata ile springi kuu kuwekwa katikati ya. . . Roho Yake katikati ya roho yako. Unaona, ulikuwa na uigaji wa uongo. Wewe, ulilia. Ulikuwa na dha—dha—dha—dhana mbaya. Unaona? Wewe, wewe tu—wewe ulikubali tu upande wa muhemko, wala hukupata upande halisi. Ulisikia tu hiyo saa ikipiga nawe ukasikia kelele, nawe ukaifuata, ukaanza kupiga, pia.

138 Lakini ikiwa hiyo springi kuu inapiga, endapo ina—inadhibiti kila mhemko, basi nira inakuwa rahisi. Wanaweza kusema, "Mnajua nini? Huyo hapo anaenda. Alikuwa kipenzi. Lakini, hebu mwangalieni sasa, nywele zake zimerudi moja kwa moja, vipodozi vyake vimetoweka. Anavaa mavazi haya yanayoonekana ya staha. . . " Simaanishi kuwa sasa kama kitu kilichotoka kwenye safina. Lakini ninamaanisha—ninamaanisha hivi, kwamba unapaswa kuvaa kwa heshima. "Mbona, alikuwa ni mrembo sana. Tungemwona amelala nje barazani, amevaa kaptura yake, akiota jua, lakini hafanyi hivyo tena." Jambo fulani limetukia. Ile springi kuu imefika mahali inapopaswa kuwa. Hiyo ni kweli. "Loo, alikuwa akishuka kuja. Alikuwa bingwa wa karata. Angeweza kucheza karata, konzi la *hizi*. Naye angeweza kuchakura vibao kutoka hapa, na kadhalika. Alikuwa ninii. . .Lakini hafanyi hivyo tena." Ile springi kuu! "Loo, yeye ni mtakatifu anayejibingirisha."

139 Lakini, nira ni nyepesi. Unajua unachofanya nayo? Unapenda tu kuibeba. Ni kama tu Samsoni alipolinyanyua lile lango la shaba la Gaza. Lile lango kubwa la shaba, alilinyanyua tu mabegani mwake na kulibeba. Hiyo ni kweli. Basi nira inapolainishwa na furaha, na amani, na utamu wa Kristo moyoni mwako, basi wewe unachukua tu mizigo yote

ambayo ulimwengu unakutwika, na kuibeba mpaka kwenye kilima fulani kiitwacho Kalvari, na hapo unapiga magoti na kumwombea yule aliyekuwa anakutesa. Sio kushusha moto kutoka Mbinguni na kulivunja kanisa, bali unawaletea amani. "Mungu, uwarehemu."

140 Sasa, Biblia ilisema, ya kwamba, "Pepo mchafu anapomtoka mtu, hutembea katika maeneo mapya kisha anarudi." Na wakati ibilisi ambaye wakati mmoja alikuteremsha kwenye uchochoro, basi anaporudi na kuona uchochoro wake wa zamani umebadilishwa; jamani, Mungu alishusha tingatinga Lake kubwa. Unajua alichofanya? Aliichimba ardhi. Akapindua vitu juu chini. Akafanya tu mtazamo tofauti wake. Na hapo ibilisi anaporudi kwenye uchochoro wake wa kale wa mabati, ambapo hapo awali alikuwa na makopo ya bia yametanda juu ya kila kitu, na karata mezani, na sehemu za sigara nyumbani kote, na magazeti ya *Hadithi za Upendo,* na *Kweli*. Anarudi na kukuta imefagiliwa, imepambwa. Haleluya! Mungu alituma buldoza Yake chini na kuisafisha yote.

141 Hii *hapa* buldoza Yake, ndugu. Hebu ilinganishe na *Hili*. Anaifagia yote, anaisafisha yote kwa buldoza, Naye anaanza kupanda bustani. Naye anapata, hapo, nyumba kubwa mpya ya kisasa, imejengwa humo. Amina.

142 Roho Mtakatifu ameingia ndani. Naye Roho Mtakatifu akapachukua mahali pa makopo ya bia. Biblia ikachukua mahali pa vitabu vya hadithi za kisasa. Roho wa Mungu akachukua mahali pa theolojia ya kisasa. Mkutano wa maombi ukarudi nyumbani, wakati Roho Mtakatifu alipoingia. Mambo mengine yote yametoweka.

143 Basi, sikiliza, ewe rafiki. Hapo mwanzo, Biblia ilisema... Tazama. Sasa nataka kuwajulisha...Wasomi wetu wote na kanuni zetu za imani za kujibunia...Ninapofunga, ninataka kuwajulisheni jambo fulani.

144 Hapo mwanzo, wakati ulimwengu huu ulipokuwa umelala hapa, utupu, haukuwa chochote ila mpira mkubwa wa maji, ambapo mito mikubwa ya barafu, na kutoka kwenye joto la jua, huku kumetameta kwa dunia kulipoondoka namna hiyo na kuhamia angani, pamoja, mamilioni chini ya sifuri. Ilifanyiza unyevu.

145 Joto na baridi, pamoja, hufanyiza unyevu. Unaweza kuuona madirishani, na kadhalika, kutoka kwenye nyumba, hapa ndani na nje.

146 Basi dunia ilipozunguka ikatoka kwenye mzingo wowote ilimotoka, ambapo, jua linadaiwa kuwa mama wa yote, na makombora haya yaliyoruka nje. Ulipotoka huko, uliganda ukawa kitu kimoja kikubwa kigumu. Ndipo, ulipoanza kuingia, na Mungu akapata wazo...Sikilizeni kwa makini

sasa. Alipoanza kuuingiza ndani, karibu na jua, ulianza kuyeyuka.

147 Ndipo, Mungu akamwagiza Roho Mtakatifu. . .Mtu wa kwanza, anatambulishwa, ni Mungu. Mungu! "Hapo mwanzo alikuwako Mungu," katika Mwanzo. Na halafu wa pili, aliyetambulishwa, ni Roho Mtakatifu, ama Logos, aliyetoka kwa Mungu. Hata hivyo, utu wote wa Mungu ndio uliotoka, ukawa Mtu. Nayo Biblia ilisema, "Akaanza kuatamia juu ya dunia." *Kuatamia* maana yake ni "kufanya mapenzi," kunong'oneza kama njiwa. Akaanza kuatamia juu ya nchi. Ikawaje?

148 Wanadamu, raia wenzetu, wanadamu wanaume kwa wanawake, kama nilivyo mimi asubuhi ya leo; wanadamu walio na nafsi, nafsi isiyopatikana na mauti iliyo ndani yako, wewe ni nani? Ulitoka wapi, na unaenda wapi? Wazia sasa hivi, kwa dakika moja.

149 Hivi majuzi usiku, wakati nanii wangu. . .Mliona kwenye gazeti. Mmoja wa binamu zangu, ambaye alikuwa muuza dawa, ama daktari, huko Louisville. Aliposhuka kwenda kazini mwake, kisha akarudi nyumbani, naye akaketi chini kula chakula chake cha jioni. Ndipo akamwomba mkewe amletee chungwa, alikakamaa akafa kwa mshtuko wa moyo; Raymond Branham. Na ndugu yake, Georgie, (binamu zangu wa damu, wote wawili; watoto wa ndugu ya baba yangu), akaenda kumwona ndugu yake. Basi akiwa njiani, akirudi, dakika tano baada ya kumwacha ndugu yake, waliona gari likiyumba-yumba, likipunguza mwendo, ndipo wakamwona mtu akianguka kitini mwake. Naye akafa kwa mshtuko wa moyo.

150 Nami nikaenda kwenye nyumba ya mazishi hivi majuzi usiku, ndipo nikamwangalia, Ndugu Doc pale, nasi tukaingia. Nami nikavitazama hivyo vyumba, kwenye ishara na maua yaliyokuwa yananing'inia ukutani na pande zote. Nami nikaangalia chini, nazo kumbukumbu zikanijia niani mwangu, kama mvulana mdogo, nikicheza na wavulana hawa, nilipokuwa tu mvulana mchanga.

151 Ndipo nikawazia, hao hapo watu, nyumba imejaa watu, na kwa bloku kadhaa usingeweza hata kuegesha gari lako, kutokana na marafiki na jamaa wakiingia mle ndani. Nikaingia mle ndani, binamu yangu, Agnes, akanishika shingoni na kuanza kupiga mayowe. Nami nilipotoka kwake, kumfariji, ndipo huyu hapa Dorothy akaja, mtoto mchanga, naye akaanza kunikumbatia na kupiga mayowe, na kusema, "Billy, tutafanya nini?"

Na kama nilivyosema, "Yuko wapi shangazi Lizzie?"

152 Kasema, "Ana mshtuko wa moyo, mbaya sana, na anaweza kufa wakati wowote," mama yake.

153 Kwa hivyo nikawazia, “Kuna nini kwa kizazi hiki kikuu cha Branham?”

154 Niliwazia jambo lile lile nilipomwona baba yangu, nilipomshika mikononi mwangu, nazo nywele zake zenye mawimbi zikaangukia mkononi mwangu, na hapo nikamwona wakati aliponiangalia na kutabasamu, nilipokuwa nikimwombea, naye akaenda kukutana na Mungu.

155 Niliwazia jambo lile lile siku chache kabla ya jambo hilo, wakati Doc, ndugu yangu pale, alipomchukua ndugu yake mwenyewe, amekatwa sana kooni, ambapo jamaa mmoja, akinywa pombe, aligonga nguzo, na kuvunja gari na kumwua. Naye akafa mikononi mwa ndugu yangu. Naye akamwona baba akishuka barabarani, kutoka kwa Bibi Kelly . . . Nyumba ya Bw. Kelly kule, akilia, huku ameshika kofia yake nyeusi kuukuu mkononi mwake. Siku chache baadaye, nimemshika mikononi mwangu, alipokuwa akifa.

156 Nilisimama pale na kukitazama kile kiti cha kale cha kupembea, bila mtu yeyote ndani yake, kikianza kupembea huku na huku, huku Ruthu shemeji yangu akienda kukutana na Mungu. Nami nikasema, “Mpenzi, niitundike picha ya Yesu hapa?”

Akasema, “Billy, hapana. Yeye yuko mbele yangu, daima.”

157 Ndipo niliposimama kando ya mke wangu, Hope, mama ya mvulana wangu, Billy, na msichana wangu mdogo, Sharon. Na nikamwona akiishika mikono yangu, huku macho yake meusi yakinitazama, naye akazungumza juu ya Mahali alipokuwa ametoka hivi punde, akatamani kurudi huko, na kuniambia, “Kamwe usikose kuihubiri Injili hii, Billy. Huelewi ni furaha ya jinsi gani kuondoka namna hii.”

158 Basi saa chache baada ya hapo, nikiweka mikono yangu juu ya kichwa cha mtoto wangu mdogo anayekufa kule, na kumweka mikononi mwa mamaye, niliposema, “Ee Mungu, najua ya kwamba unapandisha utomvu mitini, kwenye majira ya kuchipua, na kuchipusha chipukizi na matunda, na kuuficha ardhini wakati majira ya baridi kali yakiendelea. Huna budi kuwa Mungu. Nami naamini kwa moyo wangu wote kwamba Mvulana huyu wa ajabu aliyezaliwa Galilaya, miaka elfu mbili iliyopita, kwamba, alipokuwa akitembea huku na huku, kulingana na Maandiko, kwangu mimi, Yeye alikuwa ndiye Masihi aliyeahidiwa. Haijalishi wanasema nini, ninaliamini. Nami najua ya kwamba kuna Kitu ndani yangu, kinachonionyesha mambo yajayo, kwamba Kiumbe cha kimbinguni hutokea, nami huona mambo kabla hayajatukia. Na Yeye hunihadharisha na hayo. Lakini mimi hapa, bila onyo, hapa ninakabili jambo hili hapa. Huyo hapo mama amelala, maiti, pale. Na yule pale baba amelala huko nje. Na sasa ati utamchukua mtoto wangu mchanga kutoka mikononi mwangu,

Mungu? Utafanya hivyo, kumchukua mpenzi wangu?" Ndipo shuka jeusi likaanza kukunjwa mbele yangu. Nilijua alikuwa amemchukua. Kama ile springi kuu isingekuwapo hapo wakati huo!

159 Shetani akaniambia, "Sasa wewe unaonaje juu yake? Hata mtoto wako mchanga mpendwa, atamchukua kutoka mikononi mwako. Ni ukatili ulioje!" Hiyo ilikuwa ile roho mpya, hiyo ilikuwa . . . mambo yote ya kiakili.

160 Hapo nikasimama, huku mifupa yangu ikigongana. Nikawazia, "Niende wapi?"

161 "Ningetoka niende nikalewe pombe. Hujawahi kunywa pombe maishani mwako, lakini ningefanya hivyo, kwa vyovyote vile. Alikwambia usinywe, bali ningekunywa, kwa vyovyote vile. Ningemwonyesha ni nani alikuwa ni bosi."

162 Nikasema, "Shetani, siwezi. Yeye ndiye Bosi." Yote yalikuwa yamefikia kwenye ile springi kuu. Nina furaha sana kwamba kuna springi kuu.

163 Nilipopanda barabarani, naye Bw. Isler . . . Familia yangu imekwisha. Nilikuwa naenda kupanda juu . . . Nisingeweza kwenda kaburini. Nilipanda tu barabarani. Mafuriko yalikuwa tu yakishuka, si muda mrefu.

164 Ndipo Bw. Isler akaja barabarani. Akaruka kutoka kwenye gari, na kusema, "Billy, nataka kukuuliza jambo fulani. Nimekuona ukilia hapa kwenye lile hema. Nimekusikia ukihubiri. Na jinsi ulivyokuwa umechangamka sana kwa Ujumbe uliokuwa ukileta, nawe ulikuwa ukiwaletea watu. Sasa Huo unamaanisha nini kwako sasa? Je, ungali unampenda? Je, bado unaweza kusema utamtumikia?"

165 Nikasema, "Bw. Isler, kama akinipeleka kuzimu, ningali nitampenda. Kwa maana, kuna kitu Fulani kilichowekwa *humu*, unaona, ambapo si mimi tena, bali ni Yeye."

166 Nilitosheka na jambo hili, kwamba, huku wamelala katika makaburi mbalimbali, kutoka hapa, hadi kwenye Walnut Ridge, iliitawanya familia yangu, baba yangu, ndugu yangu, mke wangu, mtoto wangu, nao walikuwa wakirudi kwenye mavumbi ya ardhi walikotoka. Lakini ninatambua jambo hili, ya kwamba hapana shaka walikuwa hapa wakati ulimwengu ulipoumbwa, kwa sababu walitwaliwa kutoka ardhini. Walikuwepo hapa wakati dunia ilipoumbwa.

167 Miili yetu ilikuwa hapa kabla ya dunia kuumbwa, kwa maana sisi ni wa duniani. Yote ambayo tumeumbiwa ni kalisi, potashi, petroli, nurulimwengu, atomi, zinazotushikilia pamoja. Na kwa namna fulani, kwa Akili fulani kuu, tulifanywa hivi jinsi tulivyo. Sio tu kurundikwa kwa potashi, na kalisi, na petroli, lakini kitu Fulani kiliingia ndani na kuanza kuumba, nami nikafanywa hivyo.

168 Hapo mwanzo, Roho Mtakatifu alianza kuatamia juu ya jangwa lenye giza; kunradhi mihemko yangu; lakini wakati hapakuwapo na kitu, wala hapakupata kuwa na chochote. Lakini Roho Mtakatifu alitumwa kutoka kwa Mungu; sio msomi. Lakini Roho Mtakatifu alitumwa kutoka katika Uwepo wa Mungu, kufanya mapenzi juu ya nchi.

169 Na, tuseme, alinyoosha mbawa Zake kubwa kuizunguka nchi, na kuanza kufanya mapenzi, au kuatamia, kunong'onezea juu ya nchi. Ninaweza kuona kalisi na potashi zikija pamoja, ndipo yungiyungi dogo la Pasaka likasimama. Roho Mtakatifu akaliatamia kutoka nchini. Naye akaendelea kuatamia. Naye aliponong'onezea na kuatamia, nikaanza kuona miti ikichipuka, ndege wakaanza kuruka kutoka ardhini, wanyama wakaanza kutembea.

170 Ndipo basi akaendelea kunong'onezea, ndipo mtu akatokea, aitwaye Adamu. Naye Adamu alionekana mpweke, kwa hiyo akamtengenezea zaotuka, kisha akatoa ubavu ubavuni mwake na kumfanyia mchumba, Hawa. Naye alimpenda Adamu na akampenda Hawa. Naye anawachukua . . .

171 Nami ninaweza kumwona maskini Hawa, alipokilaza maskini kichwa chake begani mwa Adamu. Naye alikuwa kila kitu ambacho mwanamke angeweza kutarajia, na zaidi. Naye huku amelala juu ya bega kubwa, lenye nguvu la mpenzi wake, Adamu, basi wakatembea kote bustanini, labda, huenda ikawa, si—simba akanguruma. Asingeweza kuogopa, maana hapakuwapo na woga. Kwa hiyo akasema, "Mpenzi, huyo ni simba. Nitamwita. Leo, simba, njoo huku. Duma, simbamarara, njoo hapa ulale chini." Nao wakawafuata, kama paka.

172 Pepo zikaanza kuvuma, na nywele za maskini Hawa zikaanza kuvuma. Naye akasema, "Loo, upepo huo."

173 "Amani, tulia." Nazo pepo zikamtii. Alikuwa mwana wa Mungu. Mwanamke alikuwa mpenzi wake.

174 Ndipo naweza kumsikia akisema, "Mpenzi, unaona jua likitua? Wakati umewadia wa kuzungumza na Baba."

175 Kwa hiyo, wakaenda kwenye kanisa kuu, ule Mti mkuu. Na walipokuwa wakipiga magoti, kwa ghafla, Nuru ya Mbinguni, inayowaka ikashuka, ile Logos. Roho Mtakatifu aliyekuwa amewaatamia kutoka duniani, akashuka; Baba Mungu. Naye akasema, "Watoto, mmejifurahisha leo?"

"Naam, Baba."

176 "Nimeshuka kuja kuwabusu 'usiku mwema,' na kuwalaza chini mkapumzike, usiku wa leo." Akawabusu mashavuni, akawalaza chini. Hakuna kilichoweza kudhuru. Alikuwa moja kwa moja vichakani pamoja nao. Simba, akamlaza simba chini. Akawalaza Duma, simbamarara, chini. Akawalaza wote chini, kupumzika. Ndipo Baba akafurahi sana.

177 Kisha dhambi, kwa maarifa, kiakili . . . Natumai mnalipata. Kwa akili, dhambi iliingia ulimwenguni, kwa kujaribu kutafuta nuru zaidi, kupata kitu ambacho hakikuwa katika Neno la Mungu. Mungu alisema, "Siku utakapokula matunda yake, siku hiyo utakufa." Lakini Hawa alitaka kitu kipya.

178 Loo, mnaweza kuona, kutoka moyoni mwangu, kwamba mimi sijaribu kumkasirisha mtu? Ninajaribu tu kuweka wazi, hadharani, BWANA ASEMA HIVI, Neno, si lingine ila hilo; si mambo ya ajabu-ajabu, na makanisa makubwa, na mambo ya kiakili, bali kumsikiliza Yeye aliyetuatamia kutoka duniani.

Dhambi ikaingia.

179 Na sasa, enyi marafiki, kama Roho Mtakatifu alikuwa ndiye chombo pekee ambacho Mungu alitumia kutuatamia kutoka ardhini. Na tulitoka ardhini. Nasi tulikuwa hapa kabla ya nchi kuwako. Kumbukeni, hii hapa faraja kwenu ninyi watu mtakaoombewa. Ikiwa Roho Mtakatifu, kwa kuatamia, aliumba kiumbe cha kimwili, msanifu wa miili yetu ni nani?

Ee Mungu, jalia watu walione!

180 Roho Mtakatifu alikupa kidole tumbo chako, macho yako, pua yako, kinywa chako, moyo wako. Kisha akaweka roho mpya ndani yako, kisha akaja kuishi ndani yako. Usikubali, kwa vyovyote vile, mambo ya kiakili, theolojia ambazo ni kinyume na Biblia, lakini dumu tu na BWANA ASEMA HIVI. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

181 Roho Mtakatifu aliuatamia mwili Wake Mwenyewe, apate kuishi ndani yake, Yesu Kristo; wakati alipomtia Mariamu uvuli na kuumba, ama kuatamia, chembechembe ya Damu tumboni, iliyomzaa Mwana, Kristo Yesu; ambapo Mungu Mwenyewe alipata maskani, duniani, kwa muda wa miaka thelathini na mitatu na nusu. Naye akafanyika upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, kutukomboa, na kuleta upatanisho kati ya mwanadamu aliyepotea na Mungu mtakatifu, kuwabusu na kuwapatanisha pamoja. Ili kwamba, wakati wa jua kupunga, wakati jua linapotua juu ya paji la uso wetu, wakati safari ya maisha yangu imekamilika na mbio zangu zimekwisha, ninamtaka anibusu nilale, kama alivyombusu Stefano alipokuwa amekanganyikiwa kila mahali. Akasema, "Ninaona mbingu zikifunguka, na Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu." Haya basi.

182 Sasa, hilo linaweza kutokea namna gani? Na ikiwa Mungu alitufanya kile tulicho, pasipo sisi kujua kile kilichokuwa kikiendelea . . . Ikiwa Mungu aliniumba mimi, mwanadamu, na kuniweka kwenye umri wangu sahihi kabla mauti hayajaingia . . . Nilipokuwa na umri wa miaka ishirini na mitatu hivi, nilikuwa na nguvu na mwenye afya njema. Na kama Shetani hakuingilia kati . . . Alijaribu kunilemaza na kunipiga risasi, na mambo mengi. Lakini Mungu aliona hivyo . . .

183 Nawe, ulipokuwa mchanga, na ulipokuwa mrembo, ni—ninyi wanawake ambao mmezeeka. Nanyi wanaume mliokuwa vijana, na wenye nguvu, na wenye afya. Na jinsi mlivyofurahia kuwa mwanamume, na maskini mwenzako. Kama Mungu alifanya hivyo pasipo wewe kuwa na lolote la kusema ndani yake; kamwe hukusema, "Nifanye hivi." "Ni nani ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja?"

184 Lakini kama alikufanya hivyo, pasipo wewe kuwa na lolote la kusema, ni zaidi sana vipi Yeye anavyoweza, kwa kuatamia Kwake, kukupa cha—chaguo. Na uko kwenye uhuru wa kujichagulia. Unaweza kulikataa Hili, au unaweza kulikubali. Kulikataa, ni kupotea, na kubaki potashi, na kalisi, na petroli. Lakini, kulikubali, na kuwa na moyo mpya, roho mpya, na Roho Wake; sehemu ya Logos, ndani yako, ikidhibiti mihemko yako! Na anaponong'oneza kupitia Neno Lake, unanong'oneza pia, kwa kumjibu.

"Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

"Amina, Bwana."

"Mimi ni Bwana niponyaye magonjwa yako yote."

"Amina, Bwana."

185 Ni zaidi sana vipi Yeye atakuinua, ingawa mwili wako utapeperushwa kutoka mashariki hadi magharibi, na upepo! Ni zaidi sana jinsi gani huyu Roho Mtakatifu, baada ya maangamizi kamili, kwa bomu hili la atomiki litakaloanguka humu duniani moja ya siku hizi, likilipua mashimo, na kuirusha nje kupitia angani. Lakini kalisi na potashi zitabaki hapa. Ndipo Roho Mtakatifu ataatamia tena. Kila mfupa utaenda kwa mfupa, kila kiungo kitaenda kwenye kiungo, na kutakuwako na Kanisa la Mungu aliye hai litakalosimama katika siku za mwisho.

186 Marafiki, ni kwa kuatamia tu, au kunong'oneza kwa Roho Mtakatifu unapoweza kufanya jambo hilo, ambapo Mungu atawahi kuahidi kukuinua, unapoisikiliza Sauti Yake, ile Sauti ndogo tulivu, inayonena ndani ya vilindi vya nafsi yako.

187 Na, enyi marafiki, katika kufunga, dakika moja tu zaidi. Nami ninawatakeni mwe mkiwazia kwa kina na kwa dhati. Tutaondoka, siku moja. Na mbona, loo, naomba mniambie, kwa nini mjaribu kukubali chochote cha bandia, theolojia yoyote ya kanisa, mambo yoyote ya kiakili, mihemko yoyote, chochote kinyume, wakati anga za kipentekoste zimejaa Baraka ya kweli, Roho wa halisi wa Mungu anayekutawala na kukufanya kuwa Mkristo halisi. Haikubidi kuiga chochote; wewe kuwa tu mtoto wa Mungu aliye hai. Kwa nini, niambieni, kwa nini ujaribu kukubali chochote tofauti, wakati Mungu yuko tayari na anangoja, naye amekufikisha umbali huu; na kisha anajaribu kufanya mapenzi pamoja nawe, kwa njia ya Roho Mtakatifu; ungeweza—ungeweza kukubali tangazo la kanuni za imani, na kadhalika, kujaribu kukupeleka Mbinguni, au mambo fulani

ya ajabu-ajabu, mhemko wa kiakili, ambao hata hautambuliki katika Biblia?

188 Si mlipokee? Loo, enyi watu wa Mungu, nendeni magotini mwenu na kwa Mungu wenu! Mungu na aturehemu, ndilo ombi langu, tunapoomba.

189 Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, katika wakati huu tu wa uchaji, wakati labda, wakati uu huu, kunaweza kutulia juu yenu, juu ya kanisa hili, juu ya wengi hapa . . . Wazieni kwa kina. Usiache yawe ni mawazo duni. Je, unafanya mapenzi na Roho Mtakatifu? Na je, hiyo—hiyo roho iliyo maishani mwako, inapiga-piga mihemko yako, sawasawa na Biblia? Je, una uvumilivu, upole, wema? Nyenzo hazijaninii—hazijajaribiwa . . .

Sikilizeni, mnapoomba.

190 Nyenzo hazipimwi kwa wingi wake, jinsi zilivyo kubwa; jinsi kanisa lilivyo kubwa, ninamaanisha hapa, mnaona. Hazipimwi kwa wingi wake, bali kwa ubora wake. Chuma hupimwa kwa nguvu zake. Wala kanisa halipimwi jinsi lilivyo kubwa, au washiriki wangapi. Linapimwa kwa nguvu zake, kwa Biblia. Linaweza vipi kusema "amina" kwa kila ahadi ambayo Mungu ametoa? Maisha yako yanaendeleaje? Kwa wema, upole, unyenyekevu, uvumilivu? Vipi wakati kitu kinapokukasirisha? Kuna gurudumu dogo hapo, linalopigapiga moja kwa moja, linalokudhibiti. Upendo Wake unapitia moja kwa moja moyoni mwako. Je, unajaribu tu kuigiza hilo?

191 Loo, wazieni sasa. Na wakati mnapowazia kwa makini huku Roho Mtakatifu akikushughulikia, akiatamia juu yako, akisema, "Mtoto Wangu, ninazungumza nawe."

192 Sasa, katika Jina la Kristo, huku vichwa vimeinamishwa mbele za Mungu, sio mimi, utainua mkono wako? Useme, "Mungu, weka Roho Yako ndani yangu. Huu hapa mkono wangu." Mungu awabariki. Mikono mingi, mingi sana.

193 Na, Baba Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao, Roho Mtakatifu anayeatamia daima, akibembeleza, akinong'oneza, ninaomba ya kwamba Wewe, leo hii, utachukua nafasi Yako katika moyo wa kila mtu walioinua mkono wao. Wamekuonyesha kwamba wanakuhitaji. Loo, jinsi wanavyokuhitaji Wewe! Na kama wataitambua sasa, vipi kuhusu saa ambayo moyo unakataa kupiga? Vipi kuhusu saa ambayo wanahisi mivuke baridi ya kifo ikielea kuingia ndani? Ni zaidi sana vipi watakavyoitambua wakati huo! Basi sisi ni nini? Tulitoka wapi, na tunaenda wapi?

194 Na, Baba, tumechoshwa na uigaji wa maisha ya Kikristo. Umba ndani yetu, Bwana, leo hii, moyo mpya, roho mpya. Na uweke Roho Wako, kulingana na Neno la nabii Wako, katikati ya roho yetu mpya. Na ututawale kwa upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, unyenyekevu, subira, na imani. Na matunda yote ya Roho yanaweza kupatikana ndani yetu, tunapojitoa

wenyewe kwa unyenyekevu, nafsi zetu, sehemu ya ndani kabisa. Uhai unaoleta potashi hii yote ya duniani, na kalisi, na petroli, pamoja, na kuvishikilia hivyo; ukiondoka, tunarudi mavumbini. Nasi tunatoa roho zetu; tunazikabidhi Kwako. Na utuumbie ndani yetu roho iliyo nzuri. Na jalia Roho Mtakatifu, Roho Wako, atutawale, na kutuongoza na kutuelekeza, tunapoendelea na safari.

195 Wabariki watu hawa wapendwa. Ponya magonjwa katikati yetu, Bwana, pia. Na jalia tuseme, tulipoondoka kwenye jengo hili asubuhi ya leo, "Ilikuwa vema kwetu kuwa huko. Roho Mtakatifu alifanya kazi ndani yetu, ambayo itabadilisha mihemko yetu, itakayotufanya kuwa mtu tofauti na tulivyokuwa tulipoingia."

196 Fanya upya tumaini lililo katika watakatifu. Watie nguvu, Bwana, kwa ajili ya siku inayokuja. Loo, nafaka imeiva kabisa. Yesu atakuja kwa ajili ya mavuno hivi karibuni. Nami naomba baraka hii katika Jina la Yesu. Amina.

197 Nafikiri ingekuwa vyema kutulia tu, kwa muda mfupi tu, dada anapocheza piano.

> Ninakuhitaji, loo, jinsi ninavyokuhitaji.

198 Nashangaa vile Georgie alikuwa akiwaza hivi majuzi usiku, alipokuwa ndio kwanza amwache ndugu yake aliyekufa; alipokuwa akishuka barabarani na kuhisi moyo wake ukiondoka, giza likiingia mbele zake; alipokuwa akiangukia kiti mbele yake, akiwaacha mke wake na wapendwa wake?

> Kila saa ninakuhitaji;
> Loo, nibariki sasa, Mwokozi wangu,
> Naja Kwako.

Hebu tuuimbe, pamoja.

> Ninakuhitaji kila saa,
> Loo . . . (Kwa kila mtu.)
> Unapokuwa karibu.
>
> Nakuhitaji, loo, nakuhitaji;
> Kila saa mimi . . .

Hebu tumwinulie mikono yetu.

> Loo, nibariki sasa, Mwokozi wangu,
> Naja Kwako.

199 Ee Yehova mkuu, tenda kazi sasa. Mtie muhuri kila mmoja kwa Roho Wako. Weka mioyoni mwetu kile Kitu ambacho kimekosekana kwa muda mrefu sana. Utupe ushindi huo, Bwana, ushindi huo wa kushinda tunaouhitaji kwa neema sana. Je, utafanya hivyo, Baba? Tunakungojea Wewe. Na sasa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

200 Sijui sasa, je, kuna wengine hapa wa kuombewa? Mwanamke mmoja alinipigia simu kutoka New Albany, na mtu fulani . . . Je,

kulikuwa na mwanamke aliyenipigia simu kutoka New Al-. . .? Hilo ni sawa. Vema, hapa tu kuombewa, kama tu utaninii . . . wakati sisi . . .

Endelea na wimbo uliokuwa ukicheza, dada.

201 Na, halafu, moja kwa moja hapa kando, kwa ajili ya mstari wa maombi. Ikiwa mtakuwa na kicho kwa dakika chache. Pangeni mstari, upande wa kulia hapa, ili tuweze kuwaombea wahitaji.

> . . . upande wa Yordani,
> Katika bustani tamu za Edeni
> Ambapo Mti wa Uzima unachanua,
> Kuna raha kwa . . .? . . .
>
> Yesu anavunja kila pingu,
> Anapokuweka . . .

202 Tafuteni kiti, labda, kwa ajili ya huyu ndugu, kama anataka kuketi chini. Ungependa kuketi chini, ndugu?

> Nitamsifu daima, daima,
> Nitamsifu daima, daima,
> Nitamsifu daima, daima,
> Kwa kuwa Yeye huniweka huru!

203 Sasa, nini kimetokea? Hawa wanaosimama mstarini sasa, kuombewa, wamekuja kwa uchaji juu ya imani yao wenyewe, wakiamini. Wamekuja kusema kwamba ile Divai imeingia kwenye viriba vipya, kwamba wako tayari kuitikia "amina" kwa BWANA ASEMA HIVI.

204 Biblia imesema, ambayo ni BWANA ASEMA HIVI, "Mtu yeyote wa kwenu, akiwa hawezi, waiteni wazee, wawapake mafuta, na kuwaombea. Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule." Na tena, imeandikwa katika Maandiko, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wataweka mikono juu ya wagonjwa; watapata afya." Nasi tumefundishwa kufanya hivi, na kushurutishwa na Roho Mtakatifu, kwamba hili ndilo agizo la Mungu la kuwahudumia wahitaji.

205 Haimaanishi kwamba mtu binafsi, anayeomba, lazima awe mtakatifu au malaika. Ina maana kwamba huyo mtu, anayekuja, lazima awe na imani, nafsini mwao; ya kwamba Roho Mtakatifu na kunong'oneza Kwake, kwa Neno Lake, amedondosha kitu kidogo mle ndani, ambalo linawafanya waamini kwamba Yeye atawaatamia mpaka wapone.

206 Kama vile Ibrahimu wa kale, wakati Mungu alipomtokea kwa jina la El-Shaddai, kifua, kitu kama titi la mwanamke. Naye akasema, "Ibrahimu, una umri wa miaka mia moja, lakini mimi ndimi 'Mwenye matiti.' Niegemee tu, kama mtoto mchanga, na kunyonya, nami nitalithibitisha Neno Langu."

207 Naye Ibrahimu, akiwa na umri wa miaka mia moja, alilala kifuani mwa Mungu; yeye na Sara wakiwa mmoja, bila shaka,

wakaanza kujifunza na kuatamiwa, na kulikubali Neno la Mungu. Ndipo ikawaje? Mungu akamrudisha kwenye ujana, yeye na mke wake, nao wakamzaa mtoto, Isaka; ambaye kupitia kwa Isaka akaja Kristo, aliyeubariki ulimwengu. Alifanywa kuwa baba wa mataifa.

208 Kwa sababu, "Ibrahimu aliviita vitu hivyo," sikilizeni, "ambavyo havikuwako." Kisa cha uponyaji wa Kiungu, katika Ibrahimu, hakikuwa . . . Alipoikubali ile ahadi, ilichukua miaka ishirini na mitano kutokea; miaka ishirini na mitano. Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, alipewa ahadi; akiwa na mia moja, huyo mtoto akazaliwa. Lakini, kote katika muda huu wa miaka ishirini na mitano, yeye akiendelea kufanya mapenzi kwa Roho Mtakatifu aliyemwatamia akatoka ardhini, na kuliita Neno la Roho Mtakatifu, "Kweli!" Akiviita vitu vilivyopo, kana kwamba havipo, kwa sababu vilikuwa kinyume na Neno la Roho Mtakatifu. Akafanywa kijana mwanamume, akamzaa mtoto.

209 Sasa, hivyo ndivyo tunavyokuja. Sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Nasi tuliviita vitu, dalili, mateso yetu, magonjwa yetu, kana kwamba hayakuwako, kwa sababu tunatii yale ambayo Roho Mtakatifu, kupitia kwa nabii, mwonaji, amesema kuwa ni Kweli. Na watu wote katika nyakati zote, walilikubali, na wametokea sawa, kila wakati.

210 Sasa tunaita mambo haya kuwa ni "kweli," na kuyakubali kama mali yetu binafsi, na kuchumbia tena kwa Roho Mtakatifu, "Neno Lako ni kweli. Nitakataa dalili nyingine yoyote, kitu kingine chochote. Ninaamini ya kwamba utaniponya. Kwa sababu, Neno Lako, Bwana, linasema, 'Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo, naye Mungu atawainua.' Hivyo tu. Huo ndio Ukweli."

211 Nashangaa, asubuhi ya leo . . . Namjua Ndugu Jackson; nilimsikia akiitikia "amina," mahali fulani huko nyuma. Na sijui kama kuna wahudumu wengine hapa, asubuhi ya leo, wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu, ambao wangetaka kuja, wasimame pamoja nasi, kwa ajili ya watu hawa. Hao ni ndugu na dada zenu katika Kristo. Je, mngependa kuja hapa na kuomba pamoja nasi, huku mchungaji wetu akija mbele, hapa, ikiwa atawaombea wagonjwa asubuhi ya leo. Yeyote wenu nyinyi wengine, njoni, chukueni nafasi yenu hapa pamoja nasi, wakati tunapowahudumia wa—wahitaji humu jengoni asubuhi ya leo. Yeyote wenu wahudumu anayetaka kuja. Pia ninaamini nilimwona Teddy pale, muda mfupi uliopita, sijakosea. Na wahudumu wengine wowote, hata uwe ni nani, haijalishi; tuna furaha tu kuwa pamoja nawe hapa, kama wewe ni mwaminio, kuunganisha imani yako pamoja nasi, tunapowaombea wahitaji.

212 Sasa, ninataka wazee waje, Ndugu Higginbotham na wale wanaosimama hapa, ambao wangeweza kuuendeleza mstari,

tunapowaombea, nasi tutahudumu moja kwa moja.

213 Sasa, ndugu wahudumu, njoni papa *hapa*, ili. . .Ili, tutawaombea hawa watu wawili walioketi vitini, kwanza, kisha tutawahudumia wengine.

214 Na kila mtu hapa ambaye ana uhusiano mwema na Bwana Yesu, (nanyi nyote mnapaswa kuwa nao, asubuhi ya leo), nawatakeni mjiunge pamoja nasi. Vipi kama hii. . .Na huenda ikawa ni ndugu yako, dada yako, baba yako, ama mama, nawe unawataka wawe wazima. Na ni imani yako, udhihirisho wa imani yako, ukitoka kama dainamo kubwa, humu ndani, inayoshusha Utukufu wa Shekina wa Mungu, unaomtia mafuta mtu binafsi apate kuwa na imani. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno."

215 Sasa Roho Mtakatifu yuko hapa kuingiza, ama Neno la Mungu moyoni mwako, ambalo umelikubali. Halafu basi—basi, unapoliamini, unakuja.

216 Sasa wajibu wangu ni nini, na hawa wahudumu? Kuweka mikono juu yenu. "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo," alisema Mungu.

217 Ndipo mtachukua tu hilo, na kufanya mapenzi tena kwa Roho Mtakatifu. "Ee Roho Mtakatifu, Neno Lako ni kweli. Mimi si mgonjwa, tena. Ninapata tu nafuu, wakati wote. Ninakushukuru, Baba wa Mbinguni, kwa wema Wako kwangu. Ninazidi kupata nafuu, kila saa, kila saa." Angalia kinachotendeka, wakati wewe—wakati unapofanya mapenzi, unapoatamiwa tena na Roho Mtakatifu anayekuatamia, kupitia kwa Neno.

Sasa nitaomba, kisha tutakuja, tuweke mikono.

218 Sasa, Baba Mungu, Wewe unaona haja, na hakika kabisa Wewe unaweza hata na zaidi kutimiza kila haja; Wewe, uliyeweza kumtoa Danieli katika tundu la simba; na wale wana wa Kiebrania kutoka katika tanuru ya moto; ambaye ungeweza kuifungua Bahari ya Shamu, nao watu wakatembea juu ya nchi kavu; ambaye ungeweza kumfufua Lazaro katika wafu; na kumpeleka Eliya Nyumbani, katika gari la farasi. Ee Mungu, Wewe hujawahi kushindwa.

219 Basi viriba hivi vipya vyenye Divai mpya, hivi vyenye matumaini mapya na Maisha mapya, vimekuja mbele asubuhi ya leo vipate kutiwa mafuta, viwekewe mikono, katika ukumbusho wa Neno.

220 Pia, Baba, tunasimama kama wanadamu, kuweka mikono yetu, kama vile ulivyotuagiza. "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Agizo hilo ni muhimu vivyo hivyo, katika Injili, kadiri ilivyo kuihubiri Injili, "Aaminiye na kubatizwa ataokoka."

221 Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utalijalia Neno Lako litimizwe leo hii, wakati sisi, juu ya maungamo ya watu hawa, ambao wanaileta imani yao, kuijaribu dhidi ya nguvu za ibilisi, waache waende zao, wamekombolewa, kila mmoja, katika Jina la Kristo.

222 Vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa, tunapokuja mbele sasa kuwahudumia hawa.

223 Dada yetu mpendwa, katika ushirika wa Bwana Yesu. Kama wahudumu wa msalaba, sisi sasa, kama washiriki wa Kiungu wa baraka Zake katika ufufuo, katika ukumbusho wa Neno Lake, tunaomba yule mwovu akuache, katika Jina la Yesu. Na upate kuponywa. Tunaomba imani yako na isitingizike kamwe. Bali, naomba usaidie kutoka kwa Mungu, kule kuatamia kwa Roho Mtakatifu, Nguvu zako, zilizokutoa katika mavumbi ya nchi, na kutia kila kiungo mwilini mwako; Yeye anaweza hata na zaidi kukarabati kile alichokifanya, ambapo Shetani amekibomoa. Tunakukabidhi kwa Mungu, kama mwaminio, katika Jina la Mwanawe, Yesu.

224 Naye ndugu yetu, ambaye tunamwekea mikono, kwa maombi yayo hayo mbele za Mungu Baba yetu, na kwa upako wa Roho Mtakatifu, na agizo kwamba mambo haya yanapaswa kufanywa, sisi, kama wahudumu waaminio, tunawakabidhi kwa Mungu, Roho Mtakatifu, aliyewasaidia kutoka duniani, na kuweka mwilini mwako kila kiungo. Na kwa kuwa Shetani ameshuka na kuingilia kati, akauvunja mwili wako, kwa hiyo…?…Ili kwamba juu ya…?…ya watu hawa wanaoshuka kuja humu madhabahuni. Au, juu ya yoyote…?…Tunaomba ya kwamba Mungu atakupa…?… Juu ya wajibu huu mkuu. Tunaweka mikono yetu juu yako, katika kumbukumbu la Neno, bila kuujua moyo wako, bali tunaomba kwamba Mungu Mwenyezi, Yeye aliyekuatamia kutoka ardhini, atatengeneza, au atatia nguvu sehemu muhimu zilizo dhaifu, za mwili wako, na atakurudisha kwenye…afya yako kamilifu, katika Jina la Yesu.

225 Dada yetu mpendwa…?…tunaweka mikono yetu juu yako na kuomba kwamba…?…naye hatakuwa…?… Roho Mtakatifu…?…siku moja…?…kwa utukufu wa Mungu pekee. Sasa, dada yetu, tunaposimama tumeinamisha kichwa na kumwomba Mungu Mwenyezi, atume Logos tangu mwanzo…?…na hizo rangi tofauti…?…Sisi sote… sote tulimwombea huyo…?…Na sasa tunamkabidhi Roho Mtakatifu atujalie kutoa kwa Mungu…?…Kwake kanisa lisilo na doa wala…?…la siku hizo, lilimrejesha Bibi-arusi…Ee Roho Mtakatifu, jalia…?…nami ninaomba mwanamke huyu apate afya na nguvu zake tunapomkabidhi kwa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

226 Mungu Mwenyezi na mwenye nguvu zote, Yule asiye

na kikomo, aliye kila mahali, mwenye nguvu zote, Wewe unayelijaza anga lote! Tunaweka mikono juu ya dada yetu, tukimtambulisha Kwako, kwa maombi yale yale ambayo tumeomba juu ya hao wengine, kwamba Wewe utafanya mwilini mwake, kile ambacho kimekosekana na kimeibiwa na ibilisi. Na...?...kwa utukufu wa Mungu.

227 Baba Mungu, vile vile tunaweka mikono juu ya dada yetu, kwa maombi yale yale, kwamba...?...Baraka hii tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

228 Baba Mungu, juu ya mwili wa mtu huyu, ambaye, kwa uchovu wa miaka, ana mabega yaliyoinama, uso wenye makunyanzi, na ameujeruhi mwili wake. Lakini Wewe, Ee Mungu, ambaye ndiye Roho Mtakatifu anayeatamia, tunamkabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Kwamba, Roho Mtakatifu na amgeukie kwa upendo mkuu. Na jalia isababishe ndani yetu, na kumtambua kwamba Yule aliyemtoa duniani, anaweza pia kutengeneza kile ambacho ameumba!

57-0120M Uigaji Wa Ukristo
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org